UKURASA WA 21

**BAO LA HAALAND SI LA KAWAIDA - GUARDIOLA**




UKURASA WA 3

**MBU MPYA 'STEPHIE' TISHIO MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA**

UKURASA WA 3

**IMF YAONA DALILI TUENDAKO TANZANIA KUNG'ARA KIUCHUMI**




UKURASA WA 8

**KORTINI KISA KUJITAMBULISHA MWENYEJI KWENYE OFISI YA RAIS**


# Nipashe

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

Ijumaa Oktoba 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581840

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii

UTAFITI MUHIMBILI

# Maajabu ya muziki katika tiba ya ubongo

• **Wataalamu** waumiza vichwa matumizi yake ofisini, likizo za ugonjwa...*Ukurasa 5*

UKURASA WA 4

## UWEKEZAJI BANDARI DAR WAZIDI KUVUTA WATEJA

UWEKEZAJI mkubwa katika Bandari ya Dar es Salaam, umeendelea kuwavutia...

## Waziri aagiza mchakato uanze kurejesha Jiji la Dar lililovunjwa

UKURASA 2




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa (katikati), akishuhudia hafla ya utiaji saini mikataba ya ujenzi wa barabara za halmashauri tano za mkoa wa Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



# Madiwani CCM wadaiwa kupigana kura za maoni Serikali za Mitaa

UKURASA 2

**MICHEZO** **MWAMBUSI AJIPANGA KUISIMAMISHA YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Waziri aagiza mchakato uanze kurejesha Jiji la Dar lililovunjwa

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amemwagiza Katibu Mkuu, Adolf Ndunguru kukamilisha mchakato wa uanzishaji wa Jiji la Dar es Saalam, ikiwa ni miezi 45 tangu aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli alipolivunja.

Hadi Februari 24, mwaka 2021, Dar es Salaam ilikuwa Jiji hadi Magufuli alipotangaza kulivunja na kuipandisha hadhi Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kuwa Halmashauri ya Jiji.

Hayati Magufuli alitangaza uamuzi huo siku hiyo asubuhi alipokuwa akizindua barabara ya juu ya Kijazi Interchange.

Baadaye mchana ilitolewa taarifa hiyo ilitolewa na aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo, Selemani Jafo ambaye alieleza kuwa Rais Magufuli ametumia mamlaka yake chini ya kifungu cha 84 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 kufanya mabadiliko hayo.

"Aidha, mgawanyo wa mali na madeni ya iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo imevunjwa itafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 na Sheria nyingine zinazohusika," alisema Jafo wakati huo.

Jana Waziri Mchengerwa alisema hatua ya kurejesha Jiji la Dar es Salaam ni kutokana na maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa ikiwamo ujenzi wa barabara za mwendokasi na Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili (DMDP II).

Aliagiza pia kukamilika kwa mchakato wa kukamilisha mradi wa uboreshaji wa Mto Msimbazi kwa kupata wawekezaji.

Alisema eneo la hekta 57 za Mto Msimbzaji kuanzia Pugu hadi ufukwe wa Oysterbay itajengwa miundombinu ya kisasa.

"Nikueleze katibu mkuu mchakato huu, utekelezwe haraka inavyowezekana," alisema.

Jana serikali imetia saini mikataba ya ujenzi wa barabara katika halmashauri tano za Mkoa wa Dar es Salaam, kupitia DMDP II utakaojenga kilometa 250 za kiwango cha lami.

Mradi huo unaogharimu zaidi ya Sh. trilioni 1.1 utaanza kutekelezwa Desemba mwaka huu na kuhusisha kujenga na kuboresha kilomita 90 za mifereji ya maji na kujenga vituo vya mabasi tisa, masoko 18 na madampo ya kisasa matatu.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Mhandisi Humphey Kanyenye, alisema hayo mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa katika hafla ya kuitiliana saini.

Alisema kupitia mradi huo utakoanza kutekelezwa Novemba, mwaka huu, utahusisha kata 72 na wananchi milioni nne wa Manispaa za Temeke, Ilala, Kigamboni, Kinondoni na Ubungo.

Aidha, alisema gharama za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 438 sawa na Sh. trilioni 1.1 na Benki Kuu imetoa Dola milioni 385 na Serikali ya Uholanzi itatoa ruzuku ya Dola za Marekani milioni 53.

Kanyenye alisema katika mgawanyo huo, Dola milioni 295 sawa na asilimia 67, zimeenda kwenye miundombinu na Dola milioni 108 sawa na asilimia 25 zitatumika katika usimamizi wa taka ngumu.

Alisema Dola milioni 20 sawa na asilimia tano zitatumika katika uimarishaji wa taasisi na Dola milioni 15 sawa na asilimia tatu zitatumika kwa ajili ya usimamizi wa miradi.

"Makubaliano ya mkopo wa Benki ya Dunia yalitiwa saini Februari, 2024 na utekelezaji kuanza Mei 2024," alisema Kanyenye.

Alifafanua kuwa awamu ya kwanza kilomita 207 za barabara za lami zitajengwa Mkoa wa Dar es Salaam katika Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke.

Alisema pia kilometa 75.2 zitajengwa za mifereji ya maji ya mvua iliboreshwa.

Naye Waziri wa TAMISEMI), Mchengerwa akizungumza katika hafla hiyo, alimwagiza Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, kusimamia mradi huo, kwa kuwa lengo ni kuhakikisha makandarasi hawacheleweshi kazi au kupitiliza muda wa mkataba walioingia na kuhakikisha miradi yote inakamilika kama ilivyotakiwa.

Alifafanua kuwa kati ya fedha hizo Shilingi bilioni moja ni ruzuku kutoka Serikali ya Uholanzi na katika eneo la ujenzi wa barabara tayari zabuni zimeshatangazwa na kati ya hizo jana walitia saini zabuni nane na kubaki 12.

"TARURA harakisheni utiaji saini wa zabuni zilizobaki unafanyika kwa wakati, zisicheleweshwe na kusababisha miradi ikashindwa kukamilika kwa wakati," alisema.

Alisema awamu ya kwanza Sh. bilioni 190 zitajenga kilomita 93 za barabara na Sh. bilioni 290 za mkataba uliobaki itajenga kilometa 104 ambayo itasainiwa ndani ya mwezi ujao.

Aidha, alisema wanaotekeleza miradi hiyo wakiwamo mafundi, watoke mkoa huo ili kunufaisha zaidi wakazi hao ambao ndio wanufaika wakuu wa mradi.

Mchengerwa aliagiza utekelezaji wa mradi huo kutekelezwa kwa uaminifu na usimamizi wake na kuzingatia thamani ya mradi na uhitaji wa wananchi, wasipeleke mradi ambako wananchi hawana uhitaji nao.



Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Mohamed Salum, alipotembelea Banda la TASAC, wakati wa Mkutano wa 17 wa Tathmini ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi (JSTR), jijini Arusha jana. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hilo, Nahodha Mussa Mandia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani CCM wadaiwa kupigana uteuzi wagombea serikali za mitaa

**Na Waandishi Wetu**

MADIWANI wawili wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Shnyanga wamedaiwa kuchapana makonde wakati wa kura za maoni za kutafuta wagombea wa chama hicho katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Wanaodaiwa kuhusika katika tukio hilo ni Diwani wa Ibadakuli, Msabila Malale na wa Viti Maalum katika kata hiyo, Zuhura Waziri. Tukio hilo lilitokea juzi kwenye kata hiyo ya Ibadakuli, wakati wa upigaji kura za maoni kuwapata wagombea wa mitaa kupitia chama hicho.

Akizungumzia tukio hilo, Diwani Malale alisema wakati wagombea wamemaliza kunadi na wajumbe kuanza kupewa karatasi za kupiga kura, alihoji mbona kwenye mfuko wa kuweka kura zilizopigwa hawajajiridhisha kama kuna usalama. Baada ya kuhoji hivyo, mfuko huo ulikung'utwa na kuanguka kura moja ambayo imeshapigwa.

Baada ya hapo, alisema alimwona tena msimamizi wa pili wa uchaguzi huo, akiwapigia kura watu ambao hawajui kusoma wala kuandika napo akahoji ndipo Diwani Zuhura, aliyekuwa msimamizi mkuu wa uchaguzi huo, akamwambia asiwafundishe kazi na kisha kumsusia bahasha ya karatasi za upigaji kura.

Malale alisema diwani (Zuhura) alianza kumtolea maneno ya kashfa kwamba wao ndio wamechaguliwa kusimamia uchaguzi huo, yeye diwani amekwenda kufanya nini, hivyo anapaswa kuondoka. Baada ya kuambiwa maneno hayo, alisema alimjibu kwamba hapo ni kituo chake cha kupigia kura.

Alisema baada ya muda, diwani huyo akiwa na Katibu Mwenezi wa Kata ya Ibadakuli na wajumbe wengine, walikaa pembeni wakizungumza na ghafla Zuhura alimsogelea na kuanza kumwambia kwamba hamjui eti, huku na yeye akijibu kwamba hamjui ndipo ugomvi ukaanza.

"Zuhura yeye alinirukia ili kunikamata sehemu zangu nyeti (za siri) na mimi nikamkamata kumtoa wala sikumpiga, ndipo watu wakajaa na kutuamua. Hivyo ndivyo ilivyokuwa ndugu mwandishi," alisema Malale.

Diwani Zuhura alipopigwa na Nipashe kujua hali ilivyokuwa, alisema hawezi kuzungumzia suala hilo kwa sasa kwa kuwa anajisikia vibaya baada ya kupigwa na Diwani Malale.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Anold Makombe, alipotafutwa alisema alikuwa anakwenda kwenye kikao cha ndani cha CCM, hivyo atazungumza mara baada ya kikao hicho.

"Kuhusu madiwani wa chama chetu kupigana taarifa hizo sijazipata kwa undani. Nikishazipata nitazungumza vizuri," alisema Makombe ambaye hadi inafika jioni alisema bado yuko kwenye kikao hicho.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, alisema tukio la madiwani hao kupigana bado halijaripotiwa katika kituo chochote cha polisi, hivyo watatoa taarifa baada ya kuzipokea.

Katika hatua nyingine, mchakato wa kura za maoni kupitia CCM wilayani Tarime ulikamilika juzi huku baadhi ya wenyeviti waliokuwa wakitetea nafasi zao wakibwagwa.

Akizungumza baada ya mchakato huo, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, aliwataka walioshindwa katika mchakato huo kutokukata tamaa kwa kuwa bado wanayo nafasi ya kushiriki pia katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na madiwani mwakani.

**Imeandaliwa Na Marco Maduhu (SHUNYANGA), Samson Chacha (TARIME)**

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# HABARI KITAIFA

## Mbu mpya 'Stephie' tishio la mapambano dhidi ya malaria

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI dunia ikitarajia kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa wa malaria ifikapo mwaka 2030, tishio la kibaolojia na mabadiliko ya tabianchi limeibuka.

Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kutoka Wizara ya Afya, Dk. Samwel Lazaro, alisema hayo jana kuhusu hatua iliyopigwa na nchi, kupitia kituo cha redio cha Clouds FM kwamba mbu aina ya 'Anopheles stephensi', maarufu 'stephe' hadhibitiki kwa viuatilifu vilivyoko.

Alisema taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2023 inaeleza duniani kulikuwa na ongezeko la zaidi ya wagonjwa milioni tano kipindi cha mwaka 2022, ikilinganishwa na wagonjwa wa malaria kwa mwaka 2021.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mwaka 2022 kulikuwa na wagonjwa milioni 249 kulinganisha na wagonjwa milioni 244 mwaka uliopita. Hata hivyo, taarifa hiyo inaonyesha kuwa vifo vitokanavyo na malaria vilipungua kutoka 610,000 mwaka 2021 hadi 608,000 mwaka 2022.

"Duniani nchi 44 zimeshatokomeza ugonjwa huo, zikiwamo nne kutoka Afrika ambazo ni Cape Verde, Mauritius na Morocco na baadhi zikiwa kwenye hatua ya kufikia lengo hilo miaka mitano ijayo kutoka sasa.

"Kuna matishio ambayo yameibuka sasa, kabla ya wakati ambao malengo yalikuwa yanawekwa hayakuweko. Duniani kuna mbu aina mpya alianzia Asia Mashariki na amekuwa akionekana katika nchi mbalimbali, kwanza ameshindwa kudhibitika na viuatilifu tunavyovitumia sasa hivi.

"Pia mbu huyu uwezo wake wa kuambukiza malaria ni mkubwa kuliko mbu tuliokuwa nao awali, kwa miaka yote na sasa mikakati inaelekea katika kumdhibiti," alisema Dk. Lazaro.

Alisema kuna mbalimbali na kila nchi ina mikakati yake katika kutekeleza malengo na kwa Tanzania imejiwekea miaka mitano katika mipango kwa sababu nchi ni kubwa na iko mikao tisa ambayo ina kiwango cha chini ya asilimia moja.

"Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Singida, Mwanza, Songwe, Iringa na Dar es Salaam, ina kiwango cha asilimia moja cha malaria. Kwa mujibu wa utafiti wa NBS mwaka 2022, kiwango cha malaria ni asilimia 8.1 nchini lakini baadhi ya mikoa kiwango kiko juu," alisema.

"Kiwango kiko juu ikiongozwa na mkoa wa Tabora ambako kuna asilimia 23.4, ikifuatiwa na Mtwara (20), Kagera (18), Shinyanga (16) na Mara (15) wakati Geita na Kigoma ni asilimia 13," aliongeza.

WHO inaeleza kuwa ifikapo mwaka 2030 lengo ni kupunguza maambukizi ya malaria angalau kwa asilimia 90 na kupunguza viwango vya vifo vya ugonjwa huo kwa asilimia 90.

Kadhalika, lengo ni nchi kuondoa malaria kwa nchi 35 ifikapo 2030 na kuzuia kuzuka tena kwa malaria katika nchi zote ambazo hazina malaria.

Kanda ya Afrika inabeba sehemu kubwa isiyo na mzigo wa malaria duniani. Mwaka 2022, eneo la Afrika lilikuwa na asilimia 94 ya wagonjwa wa malaria (milioni 233) na asilimia 95 (580,000) ya vifo vya malaria. Aidha, watoto walio chini ya miaka mitano walichangia takriban asilimia 80 ya vifo vyote vya malaria katika eneo la Afrika, kwa mujibu wa WHO.

Kundi la watoto wachanga, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito, wasafiri na watu wenye Virusi Vya Ukimwi (VVU) au UKIMWI wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa malaria.

Nchi nne za Afrika zilichangia zaidi ya nusu ya vifo vyote vya malaria duniani kote, Nigeria asilimia 26.8, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) asilimia 12.3, Uganda (5.1) na Msumbiji (4.2).

Katika karne ya 20 pekee, malaria iliua kati ya watu milioni 150 na milioni 300, ikichukua asilimia mbili hadi tano ya vifo vyote (ripoti ya Carter na Mendis, 2002).

Wanaougua ugonjwa huo wengi ni kutoka nchi maskini zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, Asia, bonde la Amazon na maeneo mengine ya kitropiki, asilimia 40 ya wakazi wa dunia, bado wanaishi katika maeneo ambayo malaria unakosambaa.



Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka, ikiendelea katika Barabara ya Azikiwe, eneo la Posta Mpya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## IMF yaona dalili tuendako Tanzania kung'ara kiuchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na ukuaji wa Pato la Taifa, Tanzania inakadiriwa kuwa kati ya nchi 10 za juu barani Afrika katika ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025 huku serikali ikisema hatua hiyo itaongeza uwekezaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, alisema kuwa Oktoba 22 mwaka huu, Shirika la Fedha Duniani (IMF) lilitangaza Taarifa ya Hali ya Uchumi Duniani kwa mwaka 2024, ikioonesha ukuaji uchumi nchini.

"Serikali yetu inajivunia leo ina taarifa njema, tumetajwa kwamba, Tanzania inatarajiwa uchumi wake kukua kwa asilimia sita kufikia mwaka 2025 kutoka asilimia 5.1 kwa mwaka 2024 na kutokana na ukuaji wa Pato la Taifa, Tanzania inakadiriwa kuwa kati ya nchi 10 za juu Afrika katika ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na kukua kwa uchumi huo, kunatarajiwa kuwapo ongezeko kubwa la uwekezaji kwa sekta za kilimo, viwanda, utalii na kuchangia kuondoa umaskini wa mtu mmoja mmoja.

"Pamoja na kupita kwenye changamoto za UVIKO-19 na zingine duniani, bado tumeendelea kuwa imara na duniani wanaona uchumi wetu unakua kwa kasi na utaongezeka na kufikia asilimia sita kwa mwaka ujao," alisema.

**UCHAGUZI S/MITAA**

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, msemaji huyo alisisitiza wananchi kujitokeza kuhakiki orodha ya wapigakura wa uchaguzi huo, zoezi hilo litakoma Oktoba 27, mwaka huu ili kufanya maboresho yanayoruhusiwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi.

"Tujitokeze kutimiza wajibu wetu wa kikatiba na kuanzia Oktoba 26 hadi Novemba Mosi mwaka huu utakuwa ni utoaji fomu kwa wagombea, tukumbuke maneno ya waasisi wetu kwamba viongozi wazalendo wanapatikana kwenye uchaguzi, tushiriki kupata viongozi wanaofaa kwa maendeleo yetu," alisema.

Alibainisha kuwa mashirika 83 yameomba kutoa elimu ya uraia na uchaguzi na kuwasihi wafanye kama walivyoomba.

Alisema pamoja na joto la uchaguzi huo, ni muhimu kulinda amani na utulivu wa nchi.

**UHURU WA HABARI**

Msemaji huyo alisema serikali kuruhusu uhuru wa habari na kujieleza isiwe chanzo cha kuvunja miiko, maadili na sheria za nchi na kusisitiza kuwa hakuna uhuru usio na mipaka na wajibu na kwamba serikali haijabana uhuru huo.

Kuhusu mapendekezo ya Tume iliyoundwa na Rais kuangalia hali ya Haki Jinai, msemaji huyo alisema yapo maboresho yanayohitaji sheria, sera na kanuni.

"Rais ni muumini wa haki na tume ilitoa mapendekezo zaidi ya 300 namna ya kuboresha haki kwenye vyombo vyote, serikali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo na kazi inaendelea, tuipe serikali muda ifanye kazi," alisema.

Msemaji huyo alisema serikali haina uwezo wa kuingilia taratibu za uchunguzi kwenye mapendekezo ambayo yapo mamlaka za kiuchunguzi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA

*Dar es salaam Januari 10, 2024*

**TAARIFA KWA UMMA**

**NAMBA MPYA YA KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA**

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inapenda kuwafahamisha wadau wote na Umma kwa ujumla kwamba kufuatia maoboresho iliyoyafanya katika Kituo chake cha Huduma kwa Wateja (Call Centre), namba ya simu ya Huduma kwa Wateja itakayokuwa ikitumika ni ya Kampuni ya simu ya Tanzania (TTCL) ambayo ni: **023 – 221 0500.**

Kwa muktadha huo, namba zote zilizokuwa zikitumika kuwasiiana na Kituo chetu hicho cha Huduma kwa Wateja kwa ajili ya kuulizia masuala mbalimbali yahusuayo Usajili na Utambuzi wa watu ikiwa ni pamoja na kufahamu kuhusu Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) na Vitambulisho vya Taifa, zitafungwa rasmi kuanzia tarehe 28/10/2024 na badala yake namba itakayotumika ni hiyo iliyotajwa hapo juu.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Mawasiliano na Hifadhi Hati**

**Barabara ya Kilimani, S.L.P 12324, Dar es Salaam, Simu: +255734220962, Barua pepe: info@nida.go.tz, Tovuti: www.nida.go.tz**

# Uwekezaji Bandari Dar wazidi kuvuta wateja

Na Mwandishi Wetu

UWEKEZAJI mkubwa katika Bandari ya Dar es Salaam, umeendelea kuwavutiwa wafanyabiashara kuitumia kwa ajili ya kupitishia mizigo.

Miongoni mwa kampuni hizo ni ya kutengeneza magari ya Volkswagen ya Ujerumani ambayo imeonesha nia ya kuitumia bandari hiyo kusafirisha magari na vipuri inavyovitengeneza. Hatua hiyo ni baada ya kuitembelea bandari hiyo na kueleza kuridhishwa na ufanisi uliotokana na maboresho makubwa.

Rais wa Volkswagen Afrika, Martina Biene, ambaye ni Rais wa Chama cha Watengeneza Magari Afrika (AAAM), alisema hayo jana baada ya kutembelea eneo la kuhifadhia magari yanayowasili bandarini hapo kutoka nje ya nchi.

Alisema wameamua kuitembelea Bandari ya Dar es Salaam na kuangalia namna inavyofanya kazi na uwekezaji uliofanyika ili kuangalia namna ya kufanya kazi pamoja.

"Tumevutiwa sana na maboresho yaliyofanyika yakiwamo ya miundombinu ambayo yanavutia kuitumia bandari hii kwa ajili ya usafirishaji mizigo yakiwamo magari," alisema.

"Na kupitia uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam ina mchango mkubwa sana katika ukuaji wa uchumi katika bara la Afrika kwa sababu imekuwa ni kitovu cha biashara katika nchi nyingi katika bara hili," alisema.

Alisema wao ambao ni wazalishaji wa magari na vipuri katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Afrika, hivyo wanaiona bandari hiyo kichocheo kikubwa cha biashara barani Afrika.

Bienne akiwa ameambatana na viongozi mbalimbali waandamizi wa kampuni hiyo na kupokewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, alisema wamekuwa wakifanya kazi na serikali kupitia Wizara za Uchukuzi na ile ya Ujenzi katika kuboresha sera na wamevutiwa na uboreshaji uliofanyika.

"Bandari ya Dar es Salaam ni eneo muhimu kwa ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na sisi kupitia kitengo chetu cha Afrika tunaona ni eneo muhimu la kibiashara," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA baaada ya ziara hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abeid Gallus, alisema jumuiya hiyo ya watengenezaji magari kutoka Ujerumani iliamua kuitembelea bandari hiyo kuona utayari wa kuitumia kwa ajili ya kupitisha magari na vipuri vyake.

"Wamevutiwa na utendaji kazi wa bandari yetu kwa sasa kupitia maboresho mbalimbali ikiwamo muda wa kuhudumia meli baada ya kuwasili bandarini kupungua kutoka siku 30 hadi ndani ya siku saba," alisema.

Alisema kutokana na maboresho ya vifaa vya kisasa vya ulinzi na usalama, wizi wa vipuri vya magari yanayowasili bandarini hapa haupo kwa sasa na kuwapa wateja usalama wa mizigo yao yakiwamo magari hayo.

Ofisa wa Biashara wa Kampuni ya DP World iliyowekeza bandarini hapo kutoka geti 0-7, Arun George, alisema maboresho ya miundombinu yanaendelea katika idara mbalimbali ikiwamo ya kupakua mizigo ili kuleta ufanisi zaidi.

Alisema uwekezaji huo kwa kiasi kikubwa umerudisha imani kwa wafanyabiashara ambao hapo awali waliamua kutumia bandari za nchi jirani, lakini sasa hivi wanatumia tena bandari hiyo kupitisha aina mbalimbali ya mizigo ikiwemo madini aina ya Copper kwenda nchi za nje.

George alisema bandari hiyo inapokea magari 16,000 kwa mwezi, yakiwamo madogo, malori na mabasi kutoka nchi mbalimbali, zaidi Japan, na yanahudumiwa kwa muda mfupi ili kuwafikia wateja wakiwamo wanaoagiza kutoka nchi za mbalimbali za jirani zikiwamo Congo DRC, Zambia, Malawi na Burundi.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa (kushoto), akimkabidhi zawadi Rais wa Jumuiya ya Watengeneza Magari kutoka Ujerumani, Martina Biene, alipotembelea na kujionea uwekezaji na maboresho yaliyofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam, jana. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE

# Wafanyabiashara wapongeza serikali kushughulikia changamoto za kikodi

Na Mwandishi Wetu

WAFANYABIASHARA wanachama wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini nchini Tanzania (SABFT), wamepongeza serikali za nchi zote mbili kwa kushughulikia changamoto ya kero za kikodi zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa wafanyabiashara hao, uliofanyika kwa udhamini wa Benki ya Absa kwa kushirikiana na Shirika la Ndege la Afrika Kusini (SAA), Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Manish Thakrar, alisema changamoto ya kodi kutozwa mara mbili imekuwa kilio cha muda mrefu, lakini kutokana na juhudi zinazoendelea kufanywa kwa ushirikiano wa serikali za Tanzania na Afrika Kusini, chemba za biashara na wadau wengine ni imani yao hadi kufikia mwisho wa mwaka huu kero hizo zitakuwa zimeondolewa kabisa.

Alisema Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini nchini Tanzania (SABFT), lilianzishwa miaka 24 iliyopita kwa lengo kubwa la kuwaunganisha wawekezaji kutoka nchini huko na wawekezaji wa Tanzania wenye nia ya kuwekeza nchini Afrika Kusini hivyo kunufaika na fursa zinazopatikana katika pande zote mbili.

"Kipindi kutoka mwaka 1997 kupitia mpango wa ubinafsishaji, kimsingi kumekuwa na ongezeko kubwa la uwekezaji wa wafanyabiashara kutoka Afrika Kusini katika miradi mikubwa katika sekta za mawasiliano, uzalishaji, vinywaji na vyakula, hivyo kutoa fursa za ajira kwa Watanzania pia kunufaisha wafanyabiashara wa ndani.

"Natoa shukurani za kipekee kwa Benki ya Absa Tanzania kwa udhamini mkubwa katika tukio hili, lakini pia tunaipongeza benki hii kwa jinsi inavyoweka juhudi katika kutoa huduma na bidhaa pamoja na masuluhisho mbalimbali katika kusaidia mahitaji ya kifedha kwa wafanyabiashara wa Afrika Kusini na wa Tanzania," alisema Thakrar.

Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha za Kigeni wa Benki ya Absa Tanzania, Irene Rwegalulira, akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Obedi Laiser alisema, wamejipanga vizuri kuhudumia wateja wao kutoka nje ya Tanzania kwa ubunifu zaidi ikiwa na masuluhisho tofauti ya huduma za kibenki kwa wateja wadogo, wa kati na wakubwa.

"Majukwaa kama haya yana faida sana kwani sisi benki tunakuja kama kiunganishi ili tuweze kuwasaidia katika biashara zao zinazohitaji huduma za kifedha kama vile mikopo, fedha za kigeni, pamoja na ushauri wa namna bora ya kufanya biashara nchini Tanzania kulingana na taratibu na miongozo ya serikali.

"Absa inafanya biashara sambamba na lengo kuu la kuanzishwa kwake ambalo ni kuiwezesha Afrika na Tanzania ya kesho pamoja, hatua moja baada ya nyingine, huku tukiongozwa na ahadi mpya ya chapa ya benki yetu isemayo 'Story yako ina thamani' hivyo kwa kutoa huduma bora za kibenki kwa wafanyabiashara hawa, tunaamini tunasaidia kuandika story za mafanikio za wateja wetu kwa manufaa yao na maslahi mapana ya Tanzania na Afrika Kusini," alisema Irene.

Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini kwa sasa lina jumla ya wanachama 100 kutoka katika sekta mbalimbali kama vile benki, madini, mawasiliano, viwanda vya uzalishaji na maduka makubwa.

# Mabingwa umeme wa moyo waanzisha umoja kutoa huduma

Na Christina Mwakangale

MADAKTARI bingwa wa moyo wanaotoa huduma za matibabu ya mfumo wa umeme wa moyo nchini wameanzisha umoja wao ili kuziba pengo liliko kwenye upatikanaji huduma hiyo kutokana na uhaba wa wataalamu wa eneo hilo.

Umoja huo unaitwa Chama cha Madaktari Bingwa wa Upandikizaji Vifaa na Tiba ya Magonjwa ya Mfumo wa Umeme wa Moyo.

Rais wa chama hicho, Dk. Yona Gandye, akizungumza jana jijini Dar es Salaam, alisema madaktari wanaotoa huduma hiyo wameungana ili kukutanisha wadau mbalimbali duniani kujadili namna ya kutatua changamoto wagonjwa hao wamekuwa wakipitia.

Bingwa huyo wa magonjwa ya moyo pia kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) alisema wamejadiliana kuhusu changamoto katika kutoa huduma kwa kuwa, wanatambua hiyo ni moja ya huduma ambayo nchini.

Dk. Kisenge alisema sababu zinazosababisha matatizo ya mfumo wa umeme wa moyo ni pamoja na magonjwa ya mishipa ya damu ama magonjwa ya kuzaliwa nayo yanayoweza kusababisha hitilafu katika mfumo huo.

"Kuwapo wa chama hiki kutasaidia kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya katika hatua mbalimbali za kitaaluma, pia kutoa mafunzo ya namna wagonjwa hao wanatakiwa kufanya pale anapogundulika kuwa na tatizo la mfumo wa umeme wa moyo," alisema Dk. Kisenge.

Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA), Dk. Mwanaada Kilima, alisema nchi inajivunia kuanzishwa chama hicho kwa kuwa ni sehemu ya mapambano na nguvu zinazowekwa katika kupambana na magonjwa ya ndani, ikiwamo ya mfumo wa umeme wa moyo.

Dk. Mwanaada ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya ndani na mfumo wa upumuaji katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alisema jitihada za uanzishwaji chama hicho zinapaswa kuungwa mkono kwa lengo la kuwasaidia wagonjwa kupata matibabu stahiki.

HABARI KITAIFA

# Maajabu ya muziki katika tiba ya ubongo

**Na Grace Mwakalinga**

MUZIKI una faida nyingi kwa afya ya akili na kimwili, ikiwamo kupunguza msongo wa mawazo na wasiwasi, utafiti umebaini.

Imebainika kuwa kusikiliza muziki kwa utulivu hupunguza viwango vya homoni ya cortisol ambayo hushughulikia msongo wa mawazo na kuleta hali ya utulivu kimetaboliki.

Pia una uwezo wa kuboresha afya ya akili kwa kupunguza unyongevu na kuongeza hisia za furaha na motisha na hata kupunguza maumivu kimwili.

Utafiti umebaini kuwa wagonjwa wanaosikiliza muziki wakati wa matibabu ya kimwili, hupata maumivu kidogo kuliko wale wasio na muziki. Muziki unaweza kuimarisha afya ya moyo kwa kupunguza shinikizo la damu.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kwa kushirikiana na watafiti wenza kutoka Norway, chini ya Prof. Bente Elisabeth Moen, Prof. Viggo Kruger na Prof. Brynjulf Stige, wanakusudia kufanya utafiti unaohusisha namna muziki unavyoweza kutumika mahali pa kazi kama kinga ya matatizo ya mishipa na misuli (work-related musculoskeletal disorders) na hivyo kuboresha afya ya akili na kimwili mahali pa kazi.

Hatua hii inakuja wakati ambao kumekuwa na ongezeko la matatizo ya mishipa na misuli yakiambatana na matatizo ya afya ya akili, hasa miongoni mwa wafanyakazi.

Mtaalamu wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi wa MUHAS, Dk. Israel Nyarubeli, alikiri kuwa matatizo ya mishipa na misuli mahali pa kazi yamekuwa yanaongezeka hasa kwa nchi zinazoendelea kwa takribani asilimia 50 hadi 70 ya wafanyakazi wa sekta mbalimbali.

Alisema ripoti hiyo ni kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), akidokeza kuwa takribani asilimia 15 ya nguvukazi iliripotiwa kuwa na changamoto ya afya ya akili mwaka 2019 na hivyo kuhitaji mbinu madhubuti za kuzuia matatizo hayo.

Alisema tiba muziki inatumika kwa ustadi maalumu, ikiwa ni njia inayofanya kazi vizuri katika kuboresha hali ya akili, akieleza kuwa utafiti uliofanywa katika mataifa kama Norway, umeonesha ufanisi wa mbinu hiyo katika kupunguza matumizi ya dawa za maumivu na kuimarisha afya.

"Katika mkutano wa mwaka 2023, wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Bergen cha Norway walikutana na sisi (MUHAS) kujadili jinsi muziki unavyoweza kusaidia kupunguza maumivu ya misuli na mifupa, matatizo yanayoathiri wafanyakazi wengi.

"Katika kikao hicho, wataalamu walisisitiza kuwa maumivu hayo yanahusishwa na kupungua kwa tija kazini na kusababisha kuwa na likizo nyingi za ugonjwa.

"Tunahitaji kuanza utafiti kuona kama kiwango kilichowekwa na WHO, kinaweza kuwa sahihi kwa nchi yetu," alisema.

Aliongeza kuwa wanapanga kufanya utafiti zaidi kuhusu matumizi ya muziki kazini, si tu kwa wagonjwa bali pia kwa wafanyakazi wenye afya, alidai mbinu hiyo itawasaidia kuelewa jinsi muziki unavyoweza kuboresha afya na ustawi wa wafanyakazi na kuongeza kuwa wapo kwenye mchakato wa kujadili namna ya kupata ufadhili wa mradi huo wa kiutafiti ambao ni muhimu kwa afya ya wafanyakazi nchini.

Alisema kuwa timu ya watafiti kutoka Bergen na Ethiopia wakati wa mkutano wa NORHED II, ilitembelea Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ambayo imekuwa Kituo cha Ubora cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na kujionea namna sanaa za maonesho zinavyoweza kutumia muziki katika nyanja mbalimbali.

Alisema kuna fursa ya kuboresha ushirikiano baina ya TaSUBa na Idara ya Muziki ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuona namna muziki tiba unaweza kutumika mahali pa kazi bila kuathiri uzalishaji na mfumo wa kazi na ajira.

## Daraja la Mzinga kujengwa

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

SERIKALI inatarajia kujenga daraja la Mzinga lililoko kati ya Mbagala Rangitatu na Kongowe kuondoa msongamano unaotokea mara kwa mara kwa wasafiri wa mikoa ya kusini.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi wa maeneo ya Mwandege na Mwanambaya wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Pwani, ukiwamo ujenzi wa barabara.

Alisema kuwa hivi sasa serikali iko kwenye hatua ya kumpata mkandarasi kujenga daraja hilo na kuondoa foleni za mara kwa mara kwa wakazi wa maeneo ya Mbagala, Kongowe, Kisemvule, Mwanambaya na wanaotumia barabara hiyo kwenda mikoa ya kusini.

Bashungwa alisema kwamba baada ya kukamilisha ujenzi wa daraja hilo, upo pia mpango wa serikali kufanya upanuzi wa barabara kutoka Mbagala Rangitatu hadi Mwanambaya kupunguza foleni inayotokea katika maeneo hayo na kusababisha msongamano.

Waziri huyo, akikagua barabara ya Mkuranga Kisiju, alimwagiza Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara ()TANROADS) kutafuta fedha za kukamilisha Km moja ya barabara inayokwenda Kisiju ambayo imesimama kwa zaidi ya miezi tisa.

Waziri Bashungwa alisema barabara za Mkuranga ni kati ya barabara za kimkakati kutokana na kuwa kwenye maeneo ya wilaya ya viwanda, hivyo wizara inawajibika kuzijenga ili kwa urahisi maeneo ya uwekezaji yafikike.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ajali zinamaliza nguvu kazi, madereva kuweni makini

**WAKATI** tukiwa tunaelekea mwisho wa mwaka, ajali nyingi zimetokea na kumaliza uhai wa watu wengi ambao walikuwa ni tegemeo kubwa kwa taifa katika uzalishaji.

Katika miezi ya kuanzia Agosti, Septemba na sasa Oktoba ukiingia ukingoni, ajali nyingi za barabarani zimetokea na watu wengi wamepoteza maisha.

Ajali zinazoripotiwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari idadi yake inatisha na kwa kweli inaacha simanzi kubwa kwa familia.

Matukio haya ya ajali mara nyingi yakifuatiliwa unakuta ni uzembe wa madereva na kutozingatia alama za usalama barabarani.

Baadhi ya madereva wanapokuwa barabarani hawajali kama kwenye magari wanayoyaendesha wamebeba roho za watu ambao wanategemewa na familia zao.

Hata hao madereva wenyewe wanapofanya uzembe huo hawajali kuwa na wao pia wapo kwenye hatari ya kupoteza maisha.

Kila mara askari wa usalama barabarani wamekuwa wakitoa elimu ya madereva kuzingatia usalama wawapo barabarani, lakini elimu hiyo haitiliwi maanani.

Pamoja na serikali kuamuru mabasi kuwekwa vidhibiti mwendo, lakini madereva wanavichezea na wanapokuwa kwenye masafa marefu wanakwenda kwa mwendo ule ule wa hatari.

Wakati taifa likiwa bado kwenye maombolezo ya vifo kadhaa vilivyotokea kwenye ajali siku chache zilizopita, kabla machungu hayo hayajapoa, ajali nyingine imetokea na kupoteza watu kadhaa na kuacha wengine wakiwa na majeraha na baadhi kubaki na ulemavu wa maisha.

Ajali hizi zitaendelea kutokea mpaka lini, ni lini madereva watakuwa na uelewa wa kuendesha magari yao kwa kuzingatia sheria za barabarani.

Wakati mwingine dereva wa gari lingine anaweza kuwa makini kwa kufuata sheria, lakini anakuja kugongwa na dereva mzembe anayeonesha mbwembwe barabarani.

Mwendokasi mara nyingi ndio unaosababisha ajali nyingi kutokea na hii inatokana na madereva hao kutaka kuwahi ili aende tripu nyingi zaidi.

Hata maeneo ya mjini mtu anaendesha kwa mwendo wa kasi bila kujali kuwa linapotokea tatizo la dharura atashindwa kudhibiti gari lake.

Kuna wakati ilishuhudiwa gari likiwa limeparamia mti na kuning'inia juu, kila mtu aliyepita eneo lile alibaki akijiuliza imekuaje yule dereva mpaka akapanda pale juu ya mti.

Kwa kweli hali inazidi kuwa mbaya na pia safari za usiku zimeanza kuleta madhara baada ya ajali nyingi kutokea muda huo, pengine kwa madereva kuchoka na kusinzia na wengine kabla ya kuanza safari kunywa vilevi, hali inayosababisha washindwe kuendesha kwa umakini vyombo vyao.


Juzi tu tumepoteza wanakwaya watano eneo la Kirinjiko, Same mkoani Kilimanjaro baada ya kupata ajali wakati wakienda kumzika mwanakwaya mwenzao.

Inasikitisha kuona wale waliokwenda kumzika mwenzao na wao wanapoteza maisha kabla hata ya kumlaza mwenzao kwenye nyumba yake ya milele.

Sijui kwa nini ajali zinapotokea zinakuwa na kisingizio cha mwisho wa mwaka. Madereva lazima wawe makini kwa kuendesha kwa umakini. Zingatieni alama za usalama barabarani, msiendeshe kwa mwendo zaidi ya ule unaoelekezwa barabarani. Huo mwendokasi ambao dereva lengo lake ni kufika haraka matokeo yake huishia kumaliza safari kabla ya mwisho wa kituo na kupoteza maisha ya watu wasiokuwa na hatia.

Tumechoka kusikia kila siku taarifa za ajali zinazotokea na kumaliza nguvukazi ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Foleni Dar zipatiwe ufumbuzi, zinakwamisha maendeleo yetu

Na Sabato Kasika

**DAR ES SALAAM** ni mji mkubwa wa kibiashara, pilika ni nyingi, likiongoza kwa idadi kubwa ya watu nchini, kwa kuwa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, inaitaja kuwa na zaidi ya watu milioni tano.

Ukubwa wake ni mithili ya majiji mengine na miji, linakumbwa na foleni kubwa za magari barabarani ambayo ni kero kwa abiria na watumiaji wengine wa barabara na vyombo vya usafiri kwa ujumla.

Katika mazingira hayo ya foleni, watu wanachelewa kufika kwenye shughuli za uzalishaji mali, wengine hujikuta wakiwa katika hatari ya kupata adhabu za makazini, kutokana na kuchelewa kazini kila mara.

Inaelezwa kuwa foleni hiyo husababisha hasara takribani Sh. bilioni 500 kila mwaka, fedha ambazo zingejenga shule za kisasa 833. Ndivyo Rais Samia Suluhu Hassan anavyosema katika moja ya hotuba zake.

Zipo sababu kadhaa ambazo huwa zinaelezwa kuwa ni chanzo cha foleni za magari barabarani, zikiwamo ongezeko la umiliki wa magari, wingi wa watu na ukuaji wa idadi ya watu, na kuendelea kukua kwa uchumi.

Vilevile, barabara zilizoko zimepitwa na wakati huku zikiwa na miundombinu duni inayosababisha kuwapo kwa foleni kwa kuwa hazitoshelezi mahitaji ya sasa ya magari yaliyopo.

Ninadhani umefika wakati sasa kuongeza idadi ya njia za kusafiria kwa magari kwa ajili ya kupunguza msongamano au foleni hizo za magari ambazo zimekuwa zikijitokeza katika maeneo mbalimbali ya jiji. Ikiwezekana, kuwe na barabara nne ambazo wengine wanaziita 'four ways' pamoja na njia za waenda kwa miguu na baiskeli, kwani kunaweza kusaidia kupunguza foleni zilizoko sasa.

Zimejengwa daraja za juu kwa ajili ya magari kwenye baadhi ya maeneo, kuna mabasi ya mwendo wa haraka, lakini hivyo vyote vimeonekana bado havijawa suluhisho la foleni za magari Dar es Salaam.

Kuna barabara mpya za mabasi yaendayo haraka zinaendelea kujengwa ni vyema, lakini sidhani kama zitaweza kusaidia kupunguza foleni, kwa sababu hakuna miundombinu inayoweza kufanya magari yasikutane.

Ni sawa kama magari yatapishana katika madaraja, lakini yanakutana mbele ya safari na kuweka foleni. Hivyo, ni vyema kuangalia uwezekano wa kuongeza barabara za juu zisizokutanisha magari mbele ya safari.

Wakati huu ambao serikali ina mkakati wa kupunguza kero ya foleni jijini Dar es Salaam, kwa kufanya mazungumzo na kampuni ya kigeni imeonyesha nia kuwekeza mtaji wa Dola za Marekani bilioni moja (Sh.trilioni 2.7) kujenga barabara ili kupunguza foleni hizo, ni vyema kweli foleni zipungue.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ubia wa Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), David Kafulila, ni kwamba mwekezaji huyo tayari amefanya kazi za awali. Anataja kazi hiyo ya awali kuwa ni upembuzi yakinifu na uchambuzi wa kiuchumi, na sasa anataka kuingia katika Hati ya Makubaliano na Serikali, ili aweze kufanya upembuzi yakinifu kamili wa mradi huo.

Kafulila anasema kampuni ya COVEC inataka kujenga barabara 10 za mzunguko (ring roads) ikiwa ni pamoja na barabara sita za ndani (inner ring roads) na barabara nne za nje (outer ring roads).

Hivyo, mkakati huo uje matokeo chanya kwenye suala la foleni za magari, kwani zinasababisha baadhi ya watu kuamka mapema kuwa usafiri badala ya kusubiri kupambazuke.

Kwa mfano, wapo baadhi ya watu wanaingia ofisini saa mbili, lakini wanalazimika kuamka saa 11 alfajiri wajiandae ili wawahi usafiri, lakini kama kusingekuwa na foleni wanaweza kuamka hata saa moja kamili.

TANGAZO

# FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

1st Housing
Homes within your reach

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30th Sep. 2024 | Robo Mwaka iliyopita 30th June. 2024 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,571 | 1,569 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,656,967 | 3,599,442 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,287,276 | 2,845,810 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 33,983,904 | 31,335,238 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,107,515 | 1,081,751 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,767,980 | 1,767,980 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 197,088 | 210,332 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **44,003,301** | **40,842,122** |
| | | | |
| B. | B. **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 2,461,997 | 2,389,711 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 437,686 | 428,545 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 544,848 | 501,281 |
| 27 | Dhima Nyingine | 232,444 | 317,815 |
| 28 | Madeni | 21,229,109 | 18,206,372 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **24,906,084** | **21,843,724** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **19,097,217** | **18,998,398** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,454,708) | (3,273,339) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 242,478 | 143,660 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 413,616 | 232,247 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **19,097,217** | **18,998,398** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 1,288,186 | 1,296,473 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 426,384 | 360,885 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 43.40% | 46.52% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.73% | 4.08% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1325.34% | 1278.45% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77.23% | 76.72% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.18% | 92.25% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3.02% | 12.18% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 7.74% | 2.18% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30th Sept. 2024 | 30th Sept. 2023 | 30th Sept. 2024 | 30th Sept. 2023 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,501,572 | 1,196,583 | 4,225,897 | 3,348,350 |
| 2 | Gharama za Riba | (564,154) | (370,266) | (1,520,159) | (1,027,741) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **937,418** | **826,317** | **2,705,738** | **2,320,609** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (65,499) | (77,683) | (159,666) | (133,256) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **131,970** | **119,451** | **408,927** | **292,439** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 204 | 1,238 | 331 | 1,345 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 131,213 | 79,206 | 338,027 | 244,938 |
| | 6.3 Gawio | - | 36,900 | 40,100 | 36,900 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 552 | 2,106 | 30,468 | 9,256 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(887,884)** | **(760,817)** | **(2,671,814)** | **(2,254,855)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (481,319) | (398,565) | (1,474,291) | (1,189,972) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (406,565) | (362,252) | (1,197,523) | (1,064,883) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **116,004** | **107,268** | **283,185** | **224,937** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (17,186) | (6,396) | (40,707) | (18,019) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **98,818** | **100,872** | **242,478** | **206,918** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **98,818** | **100,872** | **242,478** | **206,918** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 28 | 25 | 28 | 25 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.45 | 0.46 | 1.11 | 0.95 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.23% | 0.29% | 0.57% | 0.29% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.52% | 0.54% | 1.27% | 0.54% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 83.03% | 80.44% | 85.78% | 86.29% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.48% | 2.71% | 2.48% | 2.71% |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).


**Jina na Cheo :** **Saini** **Tarehe**

Amulike E. Kamwela
**(Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu)** (Imesainiwa) .............................. 25.10.2024

Antidius Kabyemela
**(Kaimu Mkuu wa Fedha)** (Imesainiwa) .............................. 25.10.2024

Isambo Binde
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** (Imesainiwa) .............................. 25.10.2024

## KEY FINANCIAL HIGHLIGHTS




## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (30.06.2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.04.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,129,679)** | **232,247** | **-** | **95,831** | **18,998,398** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 98,818 | - | - | - | 98,818 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (181,369) | 181,369 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.06.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,212,231)** | **413,616** | **-** | **95,831** | **19,097,217** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (31.03.2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.01.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,354,925)** | **367,063** | **-** | **95,831** | **18,907,969** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 90,430 | - | - | - | 90,430 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | 134,816 | (134,816) | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.03.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,128,191)** | **232,247** | **-** | **95,831** | **18,998,398** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30th Sept. 2024 | 30th June. 2024 | 30th Sept. 2024 | 30th Sept. 2023 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **116,004** | **101,675** | **283,185** | **224,937** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 71,507 | 154,212 | 225,719 | (319,582) |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,714,165) | (2,119,590) | (6,848,094) | (4,733,165) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 72,286 | 259,542 | 581,392 | 621,247 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (49,848) | 47,935 | 445,307 | 139,927 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (8,578) | (95,967) | (275,196) | (218,045) |
| | - Kodi iliyolipwa | (17,186) | (23,521) | (40,707) | (18,019) |
| | - Mengineyo | (23,523) | (40,102) | (40,102) | 61,182 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(2,553,503)*** | ***(1,715,817)*** | ***(5,668,496)*** | ***(4,241,518)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | 40,100 | 40,100 | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 30,759 | (39,817) | (32,151) | 623,797 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (57,525) | 57,179 | (56,405) | (54,918) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(26,766)*** | ***57,462*** | ***(48,456)*** | ***568,879*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu kwenda CRDB | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | 3,022,737 | 498,079 | 5,020,386 | 1,791,603 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (50,445) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***3,022,737*** | ***498,079*** | ***5,020,386*** | ***1,741,158*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **442,468** | **(1,160,275)** | **(696,566)** | **(1,931,481)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | 2,847,379 | 4,007,654 | 3,986,413 | 6,696,939 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 0 | 0 | 0 | (10,739) |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **3,289,847** | **2,847,379** | **3,289,847** | **4,754,719** |

## TARRIF

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 18% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Restructuring/Rescheduling Fee | 1% of the restructured/ rescheduling amount |
| 7 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 8 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 9 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid from Bank or Financial Institution |
| 10 | Annual Review Fee | NIL |
| 11 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 12 | Loan Statement | TZS 20,000/- |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

**Jina:** **Saini** **Tarehe**

Charles Mugila (Imesainiwa) .............................. 25.10.2024
**Mwenyekiti**

Margaret Ikongo (Imesainiwa) .............................. 25.10.2024
**Mkurugenzi**

# Apandishwa kizimbani kisa utambulisho kufanya kazi Ofisi ya Rais - TAMISEMI

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Mbeya, Venance Ibrahim amepandishwa kizimbani kwa tuhuma za kuwatambulisha watu kwenye mtandao wa kijamii wa Facebook kuwa ni wafanyakazi katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakati si kweli.

Ibrahim pia anatuhumiwa kujipatia Sh. 805,000 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa Abel Kambi kwa madai kuwa angempatia kazi huku akijua hawezi kutekeleza jambo hilo.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Harrison Lukosi alidai juzi mbele ya Hakimu Mkuu, Rahimu Mushi, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa mshtakiwa anatuhumiwa kwa mashtaka tisa, likiwamo la kuchapisha taarifa za uongo.

Lukosi alidai kuwa katika tarehe na muda usiofahamika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia mtandao wa Facebook wenye jina la Dejira Shija na Samwel Samson, alionesha kuwa watu hao ni wafanyakazi wa TAMISEMI wakati si kweli.

Alidai kuwa katika tarehe isiyofahamika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia akaunti ya Facebook ya Deborah Shija, kwa lengo la kudanganya, alijitambulisha kama Noella Stephano. Lukosi aliendelea kudai kuwa katika tarehe isiyofahamika Julai mwaka huu, mshtakiwa huyo alitumia laini ya simu yenye majina ya Samwel Mloo na kisha kujitambulisha kama Boniface Poul ambaye ni ofisa kutoka TAMISEMI.

**Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Harrison Lukosi alidai juzi mbele ya Hakimu Mkuu, Rahimu Mushi, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa mshtakiwa anatuhumiwa**

Mshtakiwa huyo pia anakabiliwa na shtaka la kutumia laini ya simu yenye jina la mtu mwingine bila kutoa taarifa kwa mtoa huduma, akitumia simu yenye jina la Samwel Samson na kisha kujitambulisha kwa Juma Lymond Andrew, ofisa wa TAMISEMI.

Alidai kuwa Agosti 8, 2024, katika mtaa wa London, Mbeya, mshtakiwa hayo alitumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina la Samwel Samson Mloopasi kutoa taarifa kwa mtoa huduma.

Mshtakiwa huyo pia anakabiliwa na mashtaka matatu ya kujipatia Sh. 805,000 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa Abel Kambi kwa madai angempatia kazi, anayodaiwa kutenda Julai 11, 2024 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Baada ya kusomwa mashtaka hayo, mshtakiwa huyo aliyakana yote na alipelekwa mahabusu kwa kishindwa kutimiza masharti ya dhamana.



Mwakilishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) Kanda ya Kati, Alfred Nicodemus, akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari, mjini Shinyanga juzi, kuhusu Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya mwaka 2023, ili wanapokuwa wakiandika habari zao za manunuzi waandike kwa usahihi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## TBS yaikwamua shule adha matundu ya vyoo

**Na Mwandishi Wetu,** BUSEGA

SHULE ya Msingi Chamugasa iliyoko Busega mkoani Simiyu imeondokana na upungufu wa vyoo baada ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuchangia ujenzi wa miundombinu hiyo uliogharimu Sh. milioni saba.

Akizungumza juzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Meneja wa TBS Kanda ya Ziwa, Happy Kanyeka, alisema hatua hiyo ni sehemu ya shirika kuunga mkono jitihada za serikali kutatua changamoto za kijamii.

"Tunarudisha kwa jamii kile tunachokipata. Hatua hii ni sehemu ya kuwezesha juhudi na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali ili kuboresha mazingira ya wanafunzi kujifunza," alisema Kanyeka.

Kanyeka pia alitumia fursa hiyo kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule hiyo kutambua bidhaa zilizothibitishwa na TBS sambamba na kusoma taarifa zinazopatikana katika bidhaa wanazonunua kwa mahitaji mbalimbali.

"Ukitumwa dukani kununua soda, maji, madaftari na bidhaa zingine hakikisha unakagua nembo ya TBS na kusoma taarifa zilizomo hususani muda wa mwisho wa matumizi," alisema.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Redempta Missanga, aliishukuru TBS kwa kusaidia ujenzi wa vyoo shuleni hapo akisema shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 1959, bado inakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo uhaba wa vyumba vinane vya madarasa na madawati 200.

"Shule hii ina wanafunzi 678, wasichana 345 na wavulana 333, walimu wanane ambao wanawake ni watano na wanaume watatu. Tunaomba wadau mbalimbali waendelee kusaidia jitihada zinazofanywa ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia," alisema Missanga.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wakiwamo Elizabeth Mafayo, Editha Misana na Zainabu Kusekwa, waliishukuru TBS kwa kuchangia ujenzi wa vyoo vipya ambavyo vimeondoa adha waliyokuwa nayo.

"Tulikuwa na changamoto za upungufu wa vyoo, hivyo tunashukuru TBS wametusaidia kujenga vyoo vipya kwa sasa hakuna changamoto tena," alisema Mafayo.

Kaimu Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, Rhobiri Chacha, alisisitiza michango inayotolewa na wadau katika halmashauri hiyo kufanya kazi iliyokusudiwa ili kuwatia moyo kuendelea kusaidia.

# Wakulima wapewa ruzuku ya bilioni 7.3/-

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KAMPUNI ya tumbaku ya Alliance One inatekeleza mkakati wa kuwapatia ruzuku ya jumla bilioni 7.3 (dola za Marekani milioni 2.7) wakulima inaofanya kazi nao kwa njia ya mikataba ya uzalishaji na ununuzi.

Fungu hilo ambalo limeelekezwa kwa wakulima hao ni kwa miaka miwili pekee kuanzia msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24 hadi msimu wa mwaka 2024/25 na tayari Sh. bilioni 3.5 (dola milioni 1.3) zimekwishawafikia na kuwanufaisha wakulima hao nchini.

Msemaji wa Kampuni hiyo, Wakili John Magoti alisema hayo jana wakati wa ziara ya ujumbe wa watu 60, wakiwamo wabunge, madiwani na wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, mkoani Tabora, walipotembelea kiwanda cha tumbaku cha Alliance One mkoani Morogoro.

Aliwaambia kwamba fungu lililowafikia wakulima hao kwa mwaka huu, limelenga kuwaondolea mzigo wa madeni ya mikopo ya pembejeo baada ya kukumbwa na majanga ya asili, ikiwamo mvua nyingi iliyoharibu tumbaku yao, hivyo kusababisha mavuno hafifu.

Wakili Magoti alisema fungu lililosalia ambalo ni Sh. bilioni 3.8 litapelekwa kwa wakulima kwenye msimu unaokuja wa mwaka 2024/25 kwa ajili ya kuboresha mabani yao ya kukaushia tumbaku kuwa ya kisasa, ili wapunguze upotevu wa zao hilo baada ya mavuno ambao kwa kawaida upotevu ni asilimia 20 hadi 30.

Aliwaeleza wageni hao kwamba kampuni hiyo kwa kushirikiana na wadau, imejenga maghala makubwa ya kuhifadhi zao hilo mkoani Tabora ambapo pia kunafanyika ununuzi wa pamoja zao hilo kwa muda mfupi.

"Kutokana na kuwapo maghala haya ambamo tunanunua tumbaku kwa pamoja, muda wa ununuzi tumbaku sasa ni siku 44 tu tofauti na hapo awali ambapo ununuzi ulichukuwa hadi miezi sita," alisema.

Wakiwa kiwandani huko, wajumbe hao walijionea uchakataji zao hilo linalolimwa kwa wingi wilayani kwao.

Walisifu uongozi wa kampuni hiyo kwa kufanya kazi kwa ubora wa hali ya juu na kupongeza teknolojia inayotumika wakati wa uongezaji thamani zao hilo ambalo ndilo msingi wa maisha yao.

Mwenyekiti wa Halmashari ya Uyui, Shaban Katalambula, alisema ujio wao ulilenga kubaini kile wanachokisikia kuhusu kampuni hiyo kama kinaendana na uhalisia katika kiwanda chake.

"Tumeona uwekezaji mkubwa kwenye kampuni hii, na hili linatupa imani sisi viongozi na wakulima wetu kwamba hawa wamejipanga kukusanya tumbaku nyingi inayozalishwa na wakulima wetu," alisema.

Mwanaidi Ahungu, Diwani wa Viti Maalum ambaye ni mkulima kutoka kijiji cha Mbola, Kata ya Isila, alisema watakwenda kusimamia mengi kwa wakulima wenzao ili wazalishe zao bora.

Alieleza kuwa awali hawakuwa wanajua hatua ambazo zao hilo linapitishwa mpaka kuingia sokoni; walifikiri ni kazi rahisi tu.

"Baada ya ziara hii, mimi na wenzangu tunakwenda kuwa mabalozi wazuri wa viwanda hivi ili kuhimiza wakulima wazalishe zao kwa ubora na wasichanganye na uchafu wowote," alisema.

Mbunge wa Uyui, Almasi Maige, alisema kuwa kile walichokiona kiwandani, kimezidi matarajio yao. Wameona jinsi tumbaku inavyoandaliwa vizuri kabla ya kupelekwa soko la kimataifa, hivyo tumbaku ya Tanzania inakuwa na viwango kwenye soko la kimataifa.

Aliwashukuru Alliance One kwa kuwa kampuni pekee mpaka sasa ambayo imetoa msaada wa ruzuku kwa wakulima ambao wamefikwa na majanga ya mvua yaliyoathiri mavuno yao.

Akitoa shukrani, Katibu Tawala wa Halmashauri hiyo, Neema Mfugale, alisema walichokiona kinasadifu kile wanachokisikia.

"Tumbaku kwetu ni uchumi, tukitoka hapa tutakwenda kuwaambia wananchi waongeze kasi ya kuongeza uzalishaji zao hili kwani soko lipo," alisema.





# Vijana wakutana kujadili mifumo ya chakula

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

VIJANA walioamua kujiajiri katika mifumo ya chakula nchini, wamekutana kwa siku tatu jijini Arusha, kujadili kuhusu chakula, uzalishaji wake, mahali kinapouzwa na kama ni salama na kina lishe.

Kundi hilo ambalo ndilo kubwa katika jamii, linaathiriwa pia na masuala ya chakula na lishe, hasa ikizingatiwa hivi sasa chakula ni fursa kutokana na ukosefu wa ajira, huku uzalishaji wa chakula ukiwa eneo ambalo linahitaji kutazamwa kama eneo la kupata ajira na kujiongezea kipato.

Akizungumza jana na kundi hilo kutoka Taasisi ya Arusha Food Systems Youth Leaders, waliokutana kujadili kuhusu mifumo ya chakula, kama sehemu ya kuchagiza maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, Ofisa Vijana wa Shirika la Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Saddam Halfan, alisema pamoja na mambo mengine, vijana hao wanajadili na kuangalia vipi shuleni wanafunzi wanakula au hawali.

"Vijana kama sehemu ambayo ina kundi kubwa la watu, ndio wanaoathiriwa pia na masuala ya chakula na lishe. Tunapozungumza sasa hivi chakula ni fursa, tuna ukosefu wa ajira lakini uzalishaji wa chakula ni eneo ambalo linahitaji litazamwe na vijana kama eneo la wao pia kupata ajira, kujiongezea kipato. Tunaangalia vipi shuleni wanafunzi wana kula au hawali," alisema. Alisema pamoja na mambo mengine, kukutana kwa vijana hao walioamua kujikita katika mifumo ya chakula, biashara ya chakula na uzalishaji wenye tija wa bidhaa za chakula na zenye lishe, ni sehemu ya utekelezaji wa kipengele cha kujenga uwezo kwa vijana katika mifumo ya chakula, unaotokana na mradi wa NFP.

> **Katika mkutano huo, Mwanahamisi Akyoo kutoka Taasisi ya Arusha Food Systems Youth Leaders, aliitaka serikali kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa skimu ya taifa ya bima za kilimo, ili kuwa ...**

"Aidha, tunajadiliana kwa pamoja ni nini ambacho wao wanaona kinafanyika katika mifumo ya chakula na kipi ambacho wanaona kifanyike kama vijana ambao ni wanufaika wakubwa wa mifumo ya chakula, kuifanya iwe jumuishi na endelevu.

"Hili ndilo kundi ambalo wataishi na mifumo hii kwa muda mrefu zaidi lakini ni wao wanaweza kuja na suluhisho na matamanio ya kuhakikisha chakula kutakuwa na mifumo ya chakula ambayo ni jumuishi, endelevu na ya kibunifu.

GAIN tunakusudia kuwafikia watu milioni moja, lakini pia katika eneo la vijana tunafikiria kuwafikia takribani vijana 100,000 kupitia mitandao ya kijamii, warsha na mafunzo," alisema.

Katika mkutano huo, Mwanahamisi Akyoo kutoka Taasisi ya Arusha Food Systems Youth Leaders, aliitaka serikali kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa skimu ya taifa ya bima za kilimo, ili kuwa na mifumo endelevu ya uzalishaji, hasa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisisitiza kwamba kutokuwapo kwa bima hiyo kunachangia wakulima wengi wadogo, na hasa vijana kutoshiriki ipasavyo katika mkakati wa taifa wa kutokomeza utapiamlo nchini. Mradi wa Nourishing Food Pathway (NFP), unatekelezwa na Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), na unafadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU), Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Uingereza na wadau wengine kutoka taasisi binafsi.

Aidha, Faith Yustin kutoka Arusha Food Systems Youth Leaders, alisema hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuwa na mifumo endelevu ya chakula, ni kujenga mazingira rafiki kwenye kilimo na masoko, huku pia akishauri serikali itoe chakula bure shuleni kwa wanafunzi wa shule za msingi, badala ya wazazi/walezi kuchangia.

Naye Hamisi Msafiri pia kutoka Arusha Food Systems Youth Leaders, alisema ili kuwa na mifumo hiyo endelevu, serikali inapaswa kupunguza vikwazo vya ushuru kwa vijana katika uzalishaji na usafirishaji mazao ya kilimo ikolojia.



Mwenyekiti wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini na Mbunge mstaafu wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu (kushoto), akitumia usafiri wa pikipiki maarufu bodaboda, wakati akielekea katika msiba wa mmoja wa waasisi wa CCM, John Kilua (95), aliyefariki na kuzikwa katika makaburi ya mji mpya, Kijiji cha Magila, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kasi utumikishaji watoto yaongezeka

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KASI ya watoto kutumikishwa katika kambi za kufyatulia matofali ya ujenzi, imeanza kuathiri sekta ya elimu, baada ya kudaiwa kukimbilia kutafuta maisha kwenye maeneo ya Newland na Shabaha, Wilaya ya Moshi, Kilimanjaro.

Ajira hizo za watoto zimegunduliwa wakati takwimu za kitaifa zikionesha zaidi ya watoto milioni tano wanatumikishwa nchini Tanzania, huku watoto milioni 4.8 wakiwa katika ajira hatarishi.

Hayo yamo katika ripoti ya matokeo ya utafiti mdogo uliofanywa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na wanajamii wanaounda Kituo cha Taarifa na Maarifa-Kata ya Mabogini, yenye vijiji vinane ambayo imewasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Shadrack Mhagama.

"Ukatili wa kiuchumi, mfano kuna ajira za watoto zimejitokeza kwenye baadhi ya maeneo kama vile Newland kwenye makambi ya tofali. Ajira hizi au utumikishwaji huu wa watoto unawanyima fursa ya kupata elimu na haki nyinginezo kama matunzo na afya," alisema Agness Moshi, mkazi wa Newland.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, utafiti huo unaonesha sababu ya watoto kuajiriwa hasa kwenye kambi hizo ni umaskini unaozikabili familia hasa za vijijini. Pamoja na mambo mengine, ripoti hiyo imeishauri serikali kuweka mkazo kwenye utekelezaji wa mipango madhubuti ya kuimarisha uwezo wa kaya, hali ambayo itapunguza umaskini na watoto kuepukana na ajira.

Baada ya utafiti huo, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Lucas Mtulya, alisema wanafanya utafiti kujua ni maeneo gani ndani ya halmashauri hiyo yanahitaji kutungiwa sheria ndogo ili kukomesha shughuli hizo.

TGNP na Taarifa na Maarifa-Kata ya Mabogini, vimefanya utafiti wa siku tisa, pamoja na kuibua ajira ya watoto, pia umeibua ongezeko la ukatili wa kingono, hasa ulawiti kwa vijana wa kiume na ubakaji kwa wasichana wanaobakwa kwa kundi kwenye baadhi ya maeneo. Kata ya Mabogini inaundwa na vijiji vya Mvuleni, Mji Mpya, Maendeleo, Chekereni, Muungano, Mabogini, Mtakuja na Mserekia, ambapo tishio kwa ukatili wa kingono, ni kwa Manosa na Remiti, Kijiji cha Mserekia.

## Uzalishaji gesi sasa futi ujazo milioni 230

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imesema uzalishaji wa gesi nchini, umefikia futi za ujazo milioni 230 kwa siku.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia masuala ya mafuta na gesi, Dk. James Mataragio, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkondo wa Juu Udhibiti wa Petroli (PURA), uliofanyika jijini hapa.

Mataragio alisema katika kibali kilichotolewa na Wizara ya Nishati cha uendelezaji wa kitalu kipya cha Ntolya, serikali inatarajia kitaanza uzalishaji mwakani.

"Hiki kitalu kitaongeza gesi katika matumizi ya nchi na tunategemea kwamba kwa kuanza tu, kitakuwa kinazalisha futi za ujazo milioni 40 kwa siku na uzalishaji utaendelea mpaka kufikia futi za ujazo milioni 120.

"Tuko kwenye mikakati TPDC (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania), wameitisha zabuni kujenga bomba la gesi, kwa hiyo bomba lililoko pale Ntolya, litasafirisha kwenda Madimba ambako ndio kuna mitambo yetu ya kuchakata gesi," alifafanua.

Pia alisema serikali imejipanga kuhakikisha kuwa wataalamu waliopo katika sekta ya nishati ya mafuta, wanapatiwa mafunzo ya ujuzi wa mara kwa mara ili kuendana na kasi ya teknolojia.

Alisema taasisi zote ambazo ziko chini ya wizara hiyo, zina fungu la fedha kutoka kwenye mikataba ya uzalishaji na ugawanaji wa mapato, ambazo zinatumika katika kujenga uwezo. "Lengo ni kupata wataalamu wabobezi ndani ya nchi, tunaenda kuingia mikataba mikubwa, sasa hivi tunaenda kufanya majadiliano ya kuanzisha mradi kubwa wa LNG, ni vitu vinavyohitaji ujuzi mkubwa.

"Kwa hiyo kuwa na Watanzania waliobobea wataisaidia nchi kuhakikisha kwamba tunapata kazi kubwa zenye mikataba mizuri ambayo itawanufaisha wananchi kwa vizazi vingi vijavyo," alisema.

Aidha, alisisitiza ni muhimu kuwa na wabobezi, kwa kuwa watafanya kazi za ufuatiliaji na uchimbaji wa mafuta kama nchi, ambapo kwa sasa hatua kubwa imepigwa kupitia wataalamu waliopata uzoefu. "Tanzania imepiga hatua kubwa sana, miaka michache iliyopita hatutukuwa na huu uwezo lakini sasa tumejijenga mpaka kufikia shirika letu la mafuta ambalo linafanya utafutaji lenyewe na tunakwenda mpaka kwenye hatua ya kuhitaji mshirika tukishajua ardhini pana kitu.

"Zamani ilikuwa kunakuwa na kitalu bila kujua ardhini kuna nini lakini sasa hivi tunajua, kwa hiyo inatupa utayari kwamba tunaweka thamani eneo hilo kabla ya kumuita mwekezaji, hivyo hata tukijadili eneo tunajua ardhini kuna kitu gani," alisema.

HABARI KITAIFA

# Ukuaji sekta ya madini kuongeza Pato la Taifa



Waziri wa Madini, Antony Mavunde.

**Na Romana Mallya**

TUME ya Madini imesema ukuaji katika sekta ya madini utasaidia kuongeza mapato ya serikali na kukua kwa mchango wake katika Pato la Taifa (GDP) kufikia asilimia 10 ifikapo mwakani kutoka asilimia tisa ya sasa.

Imetaja mkakati mwingine ni ukusanyaji wa maduhuli na lengo la makusanyo kwa mwaka 2024/25 ni Shilingi trilioni moja sawa na wastani wa kukusanya Sh. bilioni 83.33 kwa mwezi.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Injinia Ramadhani Lwamo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa majukumu yao.

Lwamo alisema kwa sasa moja ya mafanikio kupitia sekta ya madini ni kufikia asilimia tisa ya GDP na huko nyuma ilikuwa asilimia 4.5.

"Asilimia tisa ukiangalia kwa asilimia utaona ni kidogo, lakini kiuhalisia kufikia asilimia tisa kuna jitihada kubwa zinafanyika, kama mnakumbuka miaka ya nyuma tulikuwa asilimia 4.5.

"Asilimia tisa ni kubwa na ni mafanikio makubwa tunategemea mpaka mwaka 2025 sekta hii ichangie asilimia 10. Sekta hii imeongeza uzalishaji, ajira," alisema.

Kuhusu ushirikishwaji Watanzania, Lwamo alisema jumla ya mipango 1,036 ya ushirikishwaji katika sekta ya madini iliidhinishwa kati ya 1,050.

Alisema jumla ya ajira 19,356 zilizalishwa na kampuni; 18,853 ni za Watanzania sawa na asilimia 97.40, wageni 503 sawa na asilimia 2.60.

Alifafanua kwamba kwa kiasi kikubwa nafasi za juu katika sekta ya madini katika migodi zimeshikwa na wazawa kulinganisha na huko nyuma.

"Bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 3.78 ziliuzwa migodini; kampuni za Watanzania ziliuza bidhaa zenye thamani ya Dola bilioni 3.46 sawa na asilimia 91.68; na wageni Dola bilioni 0.31 sawa na asilimia 8.32.

Alisema mwenendo chanya wa utaoji leseni za madini kuanzia mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 zilizotolewa hadi sasa ni 34,348, huku lengo likiwa ni kutoa leseni 37,318.

Alisema jumla ya leseni kubwa nne zilitolewa kwa Kampuni za Mamba Minerals Corp. Ltd, Tembo Nickel Refining Co. Ltd, Sotta Mining Corp. Ltd na Graphite Corp. Ltd.

Lwamo alisema Tume imefanya ukaguzi katika migodi mikubwa tisa ya kati (kaguzi 144) na midogo (47,535).

"Usimamizi wa stoo na maghala ya baruti; ujenzi na matumizi salama ya mabwawa ya topesumu na uhifadhi wa miamba taka; kutoa mafunzo ya usalama mahala pa kazi na utunzaji wa mazingira kwa wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo," alisema.

Alisema matokeo ya mikakati waliyojiwekea ni pamoja na kuongeza mapato na kuimarisha uchimbaji endelevu, kupungua kwa matukio ya utoroshaji wa madini, kupunguza migogoro itokanayo na mwingiliano wa maombi ya leseni na kuongeza mapato, ajira na kuwa na sekta endelevu.

Alisema mikakati waliyoiweka inalenga kutatua changamoto ikiwamo kutoa elimu, kutatua migogoro na nyingine zinazohusu vifaa vya utendaji kazi na awamu ya kwanza wamepokea magari 25.

Alisema ukusanyaji maduhuli katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 257.89 zimekusanywa.

Alisema makusanyo hayo ni sawa na asilimia 103.16 ya lengo kwa kipindi husika, na pia ni sawa na asilimia 25.79 ya lengo la mwaka 2024/2025.

Kuhusu uvamizi wa maeneo ya uchimbaji ambako watu wamepewa kwa ajili ya shughuli hizo, Lwamo alisema leseni yoyote inayotolewa kwa ajili ya uchimbaji madini, hutolewa kwa mujibu wa sheria na kutaka watu wayaheshimu.

Alisema uanzishwaji wa masoko ni baada ya wachimbaji wadogo kukosa soko maalum na katika kipindi cha nyuma utoroshaji ulikuwa mkubwa.

"Katika kupambana changamoto ya utoroshaji wa madini, ni kuwapatia wachimbaji sehemu sahihi ya kuuza madini hayo ndipo yakaanzishwa masoko.

"Kipindi hicho kampuni kubwa zilikuwa na masoko, kwa sasa hawauzi kwenye masoko, lakini sheria haijawakataza kuuza," alifafanua.

Lwamo alisema uzalishaji baada ya ukuta wa Mirerani, mafanikio ni makubwa umechangia utoroshaji madini ya Tanzanite kupungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ulinzi kufanyika saa 24.

Kuhusu kufungwa mgodi wa Buzwagi, Lwamo alisema, "Mpaka ninavyoongea kuna viwanda vinaendelea na ujenzi wa viwanda. Mwendelezo wa eneo lile unaendelea kuwa eneo la viwanda," alisema.

Alisema Tume kupitia kitengo chake cha ukaguzi migodi na mazingira kimekuwa kikifanya kaguzi za mara kwa mara kuhakikisha mgodi unapopewa leseni ya uchimbaji haichimbi nje ya mipaka ya leseni zao.

Kuhusu mikakati ya kudhibiti matumizi ya kemikali za zebaki katika migodi, alisema kwa kuendelea kutoa elimu wanaamini wachimbaji wadogo wataendelea kutumia teknolojia mbadala.


## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2024 | Robo Mwaka iliopita 30 Juni 2024 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,159.93 | 486.11 |
| 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 13,747.65 | 3,928.41 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 31,600.55 | 34,930.89 |
| 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 2,234.02 | 546.79 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 159.48 | (12.20) |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 9,886.69 | 9,249.55 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 39,584.55 | 41,861.81 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,243.21 | 1,909.89 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,195.86 | 1,343.37 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **101,811.93** | **94,244.61** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 57,489.06 | 50,177.65 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,477.44 | 1,571.15 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 705.96 | 378.06 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **59,672.46** | **52,126.87** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **42,139.47** | **42,117.75** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 169.28 | 157.47 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 8,308.32 | 8,320.13 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 831.87 | 810.15 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,139.47** | **42,117.75** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 4,120.91 | 5,475.59 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 286.64 | 306.11 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 67.92 | 66.26 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 41.39% | 44.69% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.72% | 0.73% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68.96% | 83.54% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38.88% | 44.42% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.82% | 91.88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 14.57% | 1.77% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 8.03% | 0.81% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2024 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Septemba 2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,163.33 | 2,243.10 | 6,676.48 | 6,477.12 |
| 2 | Gharama za Riba | 624.38 | 727.72 | 1,820.85 | 2,323.33 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,538.96** | **1,515.39** | **4,855.63** | **4,153.80** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 258.71 | 53.16 | 258.71 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 1.66 | (48.18) | (93.38) | 75.57 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **71.51** | **126.91** | **280.78** | **428.69** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (2.07) | 2.64 | 50.97 | 85.57 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 73.59 | 124.27 | 229.82 | 343.13 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,437.09** | **959.13** | **3,894.77** | **2,920.53** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 540.97 | 383.34 | 1,534.82 | 1,180.69 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 13.63 | 6.66 | 27.33 | 18.24 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 882.49 | 569.13 | 2,332.62 | 1,721.61 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **171.72** | **472.63** | **1,281.87** | **1,327.67** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 150.00 | 127.40 | 450.00 | 567.40 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **21.72** | **345.23** | **831.87** | **760.27** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 25 | 24 | 25 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 1 | 11 | 25 | 23 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 1 | 11 | 25 | 23 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.09% | 1.36% | 1.15% | 0.95% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.21% | 3.36% | 2.64% | 2.47% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 89.23% | 58.40% | 75.83% | 63.73% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.26% | 6.71% | 7.61% | 5.74% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2024 | Robo Mwaka iliopita 30 Juni 2024 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2024 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2023 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 21.72 | 115.92 | 831.87 | 760.27 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 356.55 | 209.04 | 650.64 | 288.05 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 2,277.26 | 1,228.47 | 7,188.18 | 2,335.94 |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | 7,311.41 | 874.20 | (589.25) | (3,791.31) |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 460.54 | 51.18 | 17.61 | 634.78 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (972.78) | 350.59 | (363.28) | (1,029.91) |
| Kodi iliyolipwa | (150.00) | (150.00) | (450.00) | (567.40) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **9,304.71** | **2,679.39** | **7,285.76** | **(1,369.58)** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (209.04) | (464.89) | (1,022.30) | (2.09) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 3,505.50 | 3,240.59 | 13,188.98 | 6,286.00 |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **3,296.47** | **2,775.70** | **12,166.67** | **6,283.91** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | (164.15) |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (76.33) | (138.37) | (214.70) | (216.55) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(76.33)** | **(138.37)** | **(214.70)** | **(380.70)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 12,524.85 | 5,316.72 | 19,237.74 | 4,533.63 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 17,671.86 | 12,355.14 | 10,958.97 | 12,085.98 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **30,196.71** | **17,671.86** | **30,196.71** | **16,619.61** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2024

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/09/2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **8,216.29** | **261.30** | **-** | **-** | **41,307.59** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 831.87 | - | - | - | **831.87** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 92.03 | (92.03) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **9,140.19** | **169.28** | **-** | **-** | **42,139.47** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 829.89 | - | - | - | **829.89** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (164.15) | - | - | - | **(164.15)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 206.39 | (206.39) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **8,216.29** | **261.30** | **-** | **-** | **41,307.59** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2024

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| RAJSHEKHAR SOMASHETT | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 24-10-2024 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 24-10-2024 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 24-10-2024 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-10-2024 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 24-10-2024 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**



Ukurasa 12

**RAS Moro: Rais katupa umeme wa viwanda, tunamjibu kwa uzalishaji**



Ukurasa 13

Nionavyo, Nyerere Day iwe Aprili 13 wakati ambao alikuja duniani


# BUFE

IJUMAA OKTOBA 25, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

**Shida ya lebo ya bidhaa sokoni, Inavyomuachia magonjwa mlaji**

UCHUMI

# Mageuzi bei korosho yalivyomletea uhai mkulima, hadi bandari Mtwara

**Na Baraka Jamali,** Mtwara



Mnada wa korosho ulivyokuwa Mtwara mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

MSIMU wa kilimo wa korosho mwaka uliopo 2024/25, mkoa Mtwara sasa una wajihi na simulizi za bashasha, katika rekodi kukionekana mageuzi makubwa ya bei; korosho ghafi ikinunuliwa bei ya juu Sh 4,195 na chini Sh. 3,060

Hayo ni mabadiliko ikilinganishwa na bei za msimu uliopita 2023/24 katika mikoa ya Mtwara na Lindi, ikiripotiwa kwa bei ya juu Sh.2190 na bei ya chini Sh. 1,250.

Katika msimu wa 2022/23, bei ya juu ilikuwa Sh.2,200 na bei chini Sh.1,520. Hivyo, kinachojiri sasa kinatajwa kuwa mabadiliko makubwa ya bei katika korosho hizo za daraja la kwanza sokoni.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho (CBT), Fransis Alfred, anaeleza kuwa ni ishara ya kuwapo uhitaji mkubwa duniani, hivyo bei za korosho zinaweza kuendelea kupanda.

Mnufaika, Rukia Silimu, mkulima kutoka kijiji cha Mwangaza wilayani Tandahimba, anayesema: "Tumepokea kwa furaha kubwa kupanda kwa bei hii, kwani haijawahi kutokea kwa miaka kadhaa iliyopita. Katika kipindi cha miaka mitatu au minne, tulikata tamaa, lakini mnada huu umetufufua sana."

Ibadi Matata, mkulima kutoka kijiji cha Nambudi kata ya Chitekete wilayani Newala, anaunga mkono hoja hiyo, akipokea kwa furaha mabadiliko ya bei ya korosho.

Ni hali inayofungua ishara nyingine ya uchumi wa umma wa wakulima, wanaotegemea zao korosho katika maisha yao na familia zao.

**BODI KOROSHO**

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho - Alfred, anaiongeza kuwa, leseni 61 zimetolewa kwa wanunuzi wa korosho msimu huu. Anafafanua kuwa katika mnada wa kwanza, kampuni 45 zilikuwa tayari na leseni na kati yao kampuni 37 zilishindana.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, kampuni 10 zilinunua korosho, huku 27 zilibaki bila kununua.

Kaimu Meneja Masoko wa Bodi ya Korosho Tanzania, Salum Khalifa, mwenendo wa minada ni mzuri.

Katika mnada wa kwanza wa Tanecu uliofanyika tarehe 11 Oktoba 2024, tani 3,933.538 ziliuzwa kwa bei ya juu ya Sh 4,440 na bei ya chini ya Sh 4,120.

Khalifa anasema: "Hii ni ishara kuwa wakulima wanahitaji kuendelea na uzalishaji, kwani soko linahitaji bidhaa zetu."

Kila mnada unaonyesha jinsi uzalishaji korosho unavyoongezeka. Kwa mfano, mnada wa Chama cha Ushirika cha Mwambao uliweza kuuza tani 3,993.538 kwa bei ya juu ya Sh 3,400 na chini Sh 3,865.

Aidha, Chama cha Ushirika cha Runali kiliuza tani 5,028.992 kwa bei ya juu ya Sh 4,150 na ya chini Sh 3,760. Katika mnada wa kwanza wa Chama cha Ushirika cha Masasi Mtwara (MAMCU) uliofanyika tarehe 14 Oktoba 2024, jumla ya tani 18,003.577 ziliuzwa kwa bei ya juu ya Sh 4,195 na chini Sh 3,440.

**WASIMAMIZI SOKO**

katika minada minne ya awali inayosimamiwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) katika mikoa ya Mtwara na Lindi, wakulima wa korosho wameingiza kiasi cha Sh 143.080 bilioni kwa mauzo ya tani 33,391

Godfrey Malekano, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMX, anathibitisha kuwa mkoa wa Lindi ulipeleka sokoni tani 11,454 zenye thamani ya Sh bilioni 48,931.

Pia, anataja mkoa wa Mtwara ukapeleka tani 21,937 zenye thamani ya Sh. bilioni 94,159 bilioni, hapo akitoa wito wakulima kufikisha korosho zenye ubora akiwa na ufafanuzi: "Bei nzuri inategemea ubora wa bidhaa..."

**RC NA BANDARI**

Katika kuimarisha mchakato wa usafirishaji korosho, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala, alitembelea bandari ya Mtwara, kukagua uhalisia ulivyo kwa shehena mbalimbali, zinazojumuisha korosho.

"Mamlaka imeamua kipindi hiki chote cha msimu, makasha yote matupu yatakuja bandarini bila kulipiwa storage. Huu ni muafaka mkubwa kwa wafanyabiashara wa korosho, kwani utarahisisha mchakato wa usafirishaji," anatamka.

Mamlaka ya Bandari Mtwara, kupitia meneja wake, Ferdinand Nyati, anafafanua kuwa gharama za kupakia na kushusha mzigo zimepungua kwa asilikia 3, huku gharama za kutumia bandari zikikadiriwa kuwa asi;imia ya gharama ya bidhaa.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

WATEULE WATATU KITAIFA, WANA ZIADA MW 91...

# RAS Moro: Rais katupa umeme wa viwanda, tunamjibu kwa uzalishaji

- Zao jipya karafuu shambani, viwanda vinakuja
- TANESCO; Kishapu MW 150 za jua; Kigoma 49.5

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ENEO moja muhimu katika mustakabali wa uwekezaji kiuchumi na mikakati yake kitaifa, huwa inahusu kuwapo uhakika wa nishati umeme.

Pia, inapotajwa dira ya uwekezaji kiuchumi, kuna maeneo ya kimkakati yanayohitaji kuwezeshewa mazingira rafiki ya ziada kufanikishwa kiuchumi, huenda baadhi yakiwa nayo kihistoria au kuandaliwa, hata kabla ya kufikiwa na upendeleo.

Sehemu mojawapo muhimu katika ufanikishaji inagusa kutoshelezwa kwa hitaji la umeme, ambayo ni nyenzo kubwa katika uzalishaji na ustawishaji kiuchumi.

Hapo ndipo Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Dk. Ally Musa Ally, anasema eneo lake limo katika mikoa mitatu kitaifa ambayo mikakati ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Morogoro imezipa kipaumbele kuhakikishiwa umeme kwa ajili ya kukuza uchumi wa viwanda kitaifa.

Hadi sasa mkoa wa Morogoro kuanzia penye mji mkuu wake Manispaa ya Morogoro na baadhi ya wilaya tayari zina viwanda, kama vile cha tumbaku, nguo na vya sukari.


Katika ufafanuzi wake, Dk. Musa anasema serikali imefanya juhudi kuwapelekea umeme hata wananchi wa Morogoro wanufaike na unaosambazwa.

Ofisa Uhusiano wa Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO), Shamu Lameck anasema Bwawa la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), mpaka sasa linatoa megawati 705 za umeme zinazoiingia kwenye gridi ya taifa na itakapokamilika, inatarajiwa kuzalisha megawati 2,115 kitaifa, ambayo ni ziada ya mahitaji nchini.

Ofisa huyo wa TANESCO anasema tayari zaidi ya shilingi trilioni 6.5 zimetumika katika mradi huo wa JHHPP, huku akitaja serikali pia inaendelea kuwekeza kwenye miradi mingine, ikiwamo eneo la Malagarasi- mkoani Kigoma, kunakotarajiwa kuzalishwa megawati 49.5.

Pia, anautaja mradi wa umeme wa jua ulioko katika mkakati wake Rais Dk. Samia ulioko mkoani Shinyanga, kwa matarajio ya kuzalisha megawati 150, utakaofanyika kwa awamu mbili, ikianza na megawati 50 na kisha megawati 100.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alipouzindua ujenzi wa mradi mnamo Machi mwaka huu, ni kwamba upo katika kijiji cha Ngunga, kata ya Talaga, wilayani Kishapu, Shinyanga.



Kazi ikiendelea katika kituo cha umeme Msamvu, mjini Morogoro. **PICHA: MAKTABA**

> **“Serikali ina matarajio makubwa na TANESCO katika kufanikisha masuala ya maendeleo ya mkoa na nchi kwa ujumla...**



Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Dk. Ally Musa Ally. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

### KINACHOENDELEA MORO

Katibu Tawala Dk. Musa, anasema mtazamo wa serikali ya Rais Dk. Samia ni kuwa na mkoa Morogoro wenye viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, vikiwamo vya ufugaji kuku vyote kwa pamoja vinahitaji umeme wa uhakika.

Anasema mategemeo ya mkoa ni kuimarisha kilimo, kwa sababu Morogoro iko juu katika sekta hiyo na sehemu ya uchumi wake, sasa wanaimarisha viwanda, kilimo nacho huingia kwa sababu ni sekta zinazotegemeana.

Kinadharia, uzalishaji kilimo unakuwa katika jozi moja na uzalishaji viwandani, kwa maana ya kupatikana malighafi ya viwanda, huku navyo vinazalisha bidhaa kwa soko la ndani na nje, huku watendaji wake na jamii pia wakipata chakula kutoka shambani.

Dk. Musa katika ufafanuzi wake, anasema kilimo pia hakiwezi kuimarika bila ya kuwapo umeme, hivyo ni lazima uwapo umeme wa hakika.

“Serikali ina matarajio makubwa na TANESCO katika kufanikisha masuala ya maendeleo ya mkoa na nchi kwa ujumla...” anasema.

Pia, ana maelezo kwamba matarajio yaliyoko ni kwamba baada ya miaka mitatu mkoa wa Morogoro utakuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha karafuu kama Zanzibar na kuna viwanda vinavyosafisha karafuu.

Pia, anasema viwanda hivyo vinahitaji kupata umeme, katika nafasi hiyo anaipongeza serikali kuhakikisha Mradi wa Umeme Vijijini (REA) unafika hadi ngazi ya chini waliko wazalishaji mmoja mmoja shambani.

Meneja wa TANESCO Morogoro, Mhandisi Fadhili Chilombe, anasema serikali imeshawekeza umeme na hakuna upungufu, huku Kituo cha Kusambaza Umeme cha Msamvu, mjini Morogoro, kikiwa na ziada ya umeme megawati 91.

Anasema, mkakati walio nao sasa ni kuhakikisha umeme unawafikia wananchi, kwa kufanya matengenezo makubwa katika maeneo mbalimbali ya usambazaji.

Mhandisi Chilombe anasema, hivi sasa wako kwenye programu ya kuboresha laini inayotokea Mikumi kwenda kituo kikubwa cha Kidatu, ili kuwahakikishia wananchi umeme.

Katika staili ya aina yake, anasema mkoa wa Morogoro umeanzisha utaratibu wa kuwaunganishia umeme wateja walio tayari laini maalum, akitaja walianza na eneo la kiwanda cha Tumbaku Alliance- One, Mkwawa.

Anasema kwa sasa, wameanza ujenzi wa laini inayopeleka umeme eneo la Mtibwa yenye urefu wa kilometa 92, utakaogharimu shilingi bilioni 10.5, kazi itakayokamilika ndani ya siku 75.

Mhandisi Chilombe anasema, kukamilika kwake kutawezesha upatikanaji umeme eneo la Mtibwa, ikisaidia usambazaji kwa wananchi wa Turiani, ambao sasa wanapata umeme kwa laini inayotumiwa mjini, hivyo wanakosa uthabiti.

### WADAU UMEME

Mdau wa umeme kutoka kampuni za kilimo cha Mkonge Zulfa Mleo, anaipongeza serikali kuboresha upatikanaji wa umeme, ikiondoa hali za hatari zilizojitokeza zamani, umeme unapokatika.

Rai yake Mleo, anaiomba TANESCO kuondoa changamoto ya kukosekana taarifa mapema za kukatika umeme inapokuwapo dharura hiyo, akisema inawasaidia kupunguza gharama za nishati umeme hiyo, kwa kampuni zinazotumia umeme kiasi kikubwa.

Mkaz wa Morogoro Mjini, Mhandisi Archard Gaetan, anaipongeza serikali kwa jitihada za kupatikana umeme wa uhakika nchini, akinena: “Sijawahi kushuhudia Tanzania ikiwa na umeme unaowaka mfululizo kama mwaka huu 2024 baada ya JNHPP kuanza uzalishaji.

Gaetan anautaja mradi huo una sura ya kitaifa, akiamini utaleta mabadiliko mengi ya uchumi nchini, akigusa baadhi ya maeneo mbali na uzalishaji, kuna uwekezaji, ujasiriamali, ajira na kodi serikali.

### UJUMBE WA BITEKO

Hivi karibuni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, aliposhiriki Wiki ya Kimataifa ya Nishati nchini Singapore, akasema Tanzania inakaribisha wawekezaji katika sekta ya nishati, waongeze kasi ya sambazaji, uzalishaji na unganishwaji wa nishati nchini.

“Serikali haziwezi kufanya kila kitu zenyewe, hivyo ni muhimu kushirikiana na sekta binafsi. Sisi Tanzania tunawaalika sekta binafsi ije kuwekeza katika sekta ya nishati, kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji, upatikanaji na usambazaji nishati na kuboresha maisha ya watu kwa ujumla,” akatamka Dk. Biteko.

Kuhusu jitihada za serikali kuimarisha sekta ya nishati nchini, Dk. Biteko, akataja miradi mbalimbali inayoendeshwa na serikali, ukiwamo wa kufua umeme la Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2115.

“Serikali inaendeleza vyanzo vipya vya nishati mfano umeme wa jua, upepo na gesi, aidha kwa sasa asilimia 51 ya umeme unazalishwa kwa maji. Tanzania tumeendelea na maandalizi ya kuuza umeme nchi za Kenya, Rwanda, Burundi.

“Sasa tunaendelea na mradi kwa ajili ya kuunganisha na nchi ya Zambia, kupitia Umoja wa Mauzio ya Umeme wa pamoja katika nchi za Afrika Mashiriki na Jumuiya za Kusini mwa Afrika (SADC). Tuna soko la uhakika, hivyo tunawakaribisha wawekezaji kuja kushirikiana nasi,” akasisitiza Dk. Biteko.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Nionavyo, Nyerere Day iwe Aprili 13 wakati ambao alikuja duniani





**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

KATIKA makuzi yangu ya miongo kadhaa sasa, nimeshuhudia watu wakizaliwa na wengine kufa. Nimeshuhudia wanapozaliwa watu, wazazi wao huhifadhi tarehe ya kuzaliwa na hata wanapofariki dunia, pia ndugu huhifadhi tarehe.

Kwa wanaozaliwa hufanyika hilo kwa ajili ya kumbukizi ambayo huendana na sherehe au hafla, siku ambayo bahati mbaya sana imepewa jina la

Kiingereza; ‘Hepi Besi Dei’ (Happy Birth Day), ambayo watu hujiandaa na kukata keki, kula na kunywa.

Siku nyingine hii isiyo na jina la Kiingereza, pengine ingeitwa ‘Happy Desi Day (Happy Death Day)’, hukumbukwa, lakini haina mashamshamu ya keki, kula na kunywa na kushangilia kama hiyo nyingine ya HBD! Kwanini? Pengine ni kutokana na majonzi. Lakini wanasema zote ni sherehe.

Watanzania tumekuwa tukiyafanya haya siku zote, tukishiriki sherehe hizo kwa namna moja au nyingine, zikitofautiana kutokana na kipato, pia mazingira na muktadha unaokuwapo wakati wa sherehe hizo, hususan ya kuzaliwa.

Mnamo Oktoba 14, 1999, Rais Benjamin Mkapa alipotangaza kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliyefariki akiwa Uingereza, nchi nzima ilizizima pamoja na majirani, pia ulimwengu wote ulishituka, kutokana na umaarufu aliyokuwa nao.

Tulimzika na kujipa pole, hata kuamua kuwa Oktoba 14 ya kila mwaka, basi iwe ni kumbukizi yake kitaifa, kwani ndiyo njia ya kumuenzi huku tukiamini na kutenda aliyoyaamini.

Ili kuongeza nguvu, tukaunganisha na kuzima Mwenge kukamilisha mbio zake nchi nzima.

Tulifanya hivyo, tukiamini kwamba kumbukizi itakuwa na nguvu, ili watu wasimsahau mapema kiongozi huyo.

Ni kwamba ikifika siku hiyo, tumkumbuke kwa sala na mengine, pia tushangilie kuzima Mwenge kwa sherehe kubwa.

Tumeendelea kufanya hivyo na mpaka siku ya Oktoba 14 mwaka huu, tukafanya hivyo jijini Mwanza kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, kwa sherehe kubwa sana iliyojaza watu pomoni nje na ndani ya uwanja, mpaka mshereheshaji akasema “Mwanza imeitika.”

Kwa aliyekuwapo akishuhudia sherehe ile, bila shaka aliona jinsi siku hiyo ambayo imekuwa akiitwa ya Nyerere, ilivyogubikwa shamrashamra za Mwenge, kumbe siku ya kifo ikageuka kama ya kuzaliwa kwa Mwalimu.

Walioelewa, wakaibuka na kuhoji kwanini siku ya Nyerere isiwe aliyozaliwa yaani Aprili 13? Kwani alizaliwa Aprili 13, 1922, sasa kwanini tushangilie ‘Death Day’ badala ya ‘Birth Day’? Vinginevyo, Mwenge uzimwe siku nyingine na si Oktoba 14, hiyo aachiwe Mwalimu kukumbukwa.

Kwa mashuhuda, siku ile pale Kirumba, kilichojitokeza na kutawala ni Mwenge, isipokuwa picha moja ya Nyerere iliyobebwa na maandamano ya vijana 1,000 waliotembea kwa miguu kutoka Butiama mpaka Mwanza, kukumbuka siku ya kifo cha Mwalimu Nyerere.

Kwingineko, tulishuhudia halaiki ya Mwenge, sare maalumu za Mwenge zenye picha ya Mwenge bila picha ya Mwalimu Nyerere aliyekuwa na siku yake, hotuba kuhusu mbio za Mwenge,na kauli kidogo kumhusu Mwalimu.

Kwa kuwa siku ya Nyerere, tulitazamia basi hata familia yake angalau ipate kijifursa cha kutoa salamu, lakini hatukuliona hilo, bali tukaishia maandamano ya sungusungu na nyimbo za wasanii wa kizazi kipya, ambao baadhi yao pengine hata hawakupata kumwona Nyerere.

Ni kawaida kuwa sherehe za ‘Birth Day’ huweza kufanyika kokote, iwe nyumbani au hata hotelini na kwingineko, ili mradi kuna keki, chakula na kinywaji, lakini ‘Death Day’ itafanyika kama si nyumbani, basi makaburini ambako wafiwa huenda kuzuru kaburi kuliombea na kulisafisha.

Lakini ya Nyerere hufanyikia kokote kunakozimwa Mwenge, huku kaburi lake likibaki kutembelewa na ndugu na jamaa wa karibu, sisi wengine tukisikiliza nyimbo za ‘Koma Sava (Comment ca va)’ na mengine tofauti!

Unajiuliza hivi kweli siku hiyo kama kweli tulikuwa na lengo la kumkumbuka na kumuenzi Baba wa Taifa, tulishindwa kutafuta vikundi vya bendi au kwaya vilivyotunga, kuimba na kurekodi nyimbo za kumsifu Mwalimu, badala ya ‘singeli’ zenye maneno tofauti au hazihusiani?

Yawezekana hatujipangi au tunaacha tu bora liende, ili mradi...! Hatutamuenzi Mwalimu kwa usahihi zaidi, kama tutaendelea na utaratibu wa kumpunguzia nafasi na sehemu kubwa inakuwa na Mwenge. Dawa naona ni kutenganisha siku hizo, kila jambo lifanyike siku na mahali pake tofauti.

Hiyo itatufanya tukae chini na kutafakari aliyofanya Nyerere kwa nchi hii na kuyafuata, kama kweli tunataka au tumedhamiria kwa nyoyo za dhati, badala ya kuendekeza yaliyo tofauti. Tutafakari, itakuwaje Oktoba 14 mwakani!

BIASHARA

# Shida ya lebo ya bidhaa sokoni inavyomuachia magonjwa mlaji

**Na Joyce Lameck**

KUTOKA katika kongamano la Mpango wa Taifa Kuzuia na Kudhibiti Magomjwa Yasiyoambukiza, lililofanyika Novemba, 2023, Meneja Mpango huo, Valeria Milinga, anasema kuna ongezeko la asilimia 9.4 kwa magonjwa yasiyoambukiza ikilinganishwa na miaka mitano ya nyuma.

Ikielezwa na matabibu wa magonjwa hayo, mufumo mbaya wa maisha ni sababu kubwa ya magonjwa yasiyoambukiza, pia ulaji vyakula kiholea.

Dk. Mashili anafafanua kuwa, magojwa ya moyo pamoja na figo ndio ambayo yanaweza kwenda kuibua magonjwa mengine katika mwili wa binadamu, kutokana na kuchukuwa nafasi, pia ufanyaji kazi wake ni mkubwa.

Aidha anasema takwimu zinaonesha kwa mwaka Duniani asilimia 70 ya vifo vinatokana na magonjwa yasiyo ambukizwa, ikiwana Tanzania ni asilimia 34.4 kila mwaka watu hupoteza maisha huku chanzo ikiwa ni magonjwa yasiyo ambukizwa.



Bidhaa zikiwa dukani ambazo lebo zake zina tafsri pana kwa ustawi wa afya. **PICHA: MTANDAO**

### WANASHERIA NA YAO

Utumiaji bidhaa bila kuwa na lebo yenye kuonekana vizuri na kueleweka nma mchanganyiko wa vitu vya aina gani, vinasaidia nini katika kujenga afya ya mtumiaji, ikiwa sababu kubwa ya kumfanya mlaji kupata madhara kiafya.

Wadau wanadai kuwa, uwekaji wa lebo zenye rangi na zinazoinekana kwenye bidhaa mbalimbali, zinamfanya mlaji kuwa na uamuzi sahihi a kufahamu faida na hasara kiafya, ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukizwa.

Vilevile wanahitaji maboresho hayo kwa wazalishaji wa bidhaa kuweka lebo kmbele ya kifungashio na zenye kuonesha vitu vilivyotumika katika uzalishaji kama vili sukari, chumvi na mafuta. Mjumbe wa Bodi ya Wakurungezi ya Chama cha Wanasherea Wanawake Tanzania (TAWLA), Wakili Vicencia Fuko, anasema vyakula vingi vilivyo pakiwa ndivyo huleta magonjwa yasiyoambukiza kwasbabu vimetengenezwa na chumvi, sukari pamoja na mafuta mabaya.

Pia anasema katika utengenezaji wake, utafiti unaonesha kuwa pindi vinapochakatwa vipo vitu vizuri hutolewa na vibaya vingi huongezwa, ili kumvutia mteja na kufanya ushindani wa viwanda ambavyo huzalisha bidhaa za kufanana.

Lengo ni kuwataka wazalishaji wa bidhaa za vyakula nchini, kuweka lebo zenye kuonesha rangi kama vile nyekundu, kijani na njano, ambazo zitamfanya mtumiaji kufanya uchaguzi sahihi ili kulinda afya yake.

Vilevile anaeleza namna bidhaa za asili zinavyoandaliwa kwa gharama, ukilinganisha na bidhaa zinazozalishwa viwandani, hiyo ndio sababu watu walio wengi wanashindwa kumudu vyakula vya asili na kujikuta wanatumia bidhaa ya ambazo tayari zimechakatwa viwandani.

Akifafanua Wakili huyo, inapaswa mlaji afanye maamuzi ya kutumia bidhaa, ambayo anafahamu faida na athali za matumizi yake, hivyo maboresho ya lebo katika bidhaa ni lazima iyonekane vizuri, iwe rahisi kueleweka pia ijirudie katika bidhaa.

Wakili na Maratibu wa Miradi wa Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Isabela Inchimbi, anasema kama chama wapo kwenye mradi wa kushawishi serikali kuwa na kanuni za lazima za viwango, ili kuhakikisha bidhaa zinazouzwa zinakuwa na taarifa kamili na kwa lugha nyepesi.

Hii ni kutokana na taarifa ya WHO kuwa vifo vitokanavyo na magonjwa yasio ambukizwa kuongezeka ukilinganisha na miaka ya nyuma, hivyo wanaamini kupitia uboreshaji wa kanuni itasaidia kupunguza idadi ya wagonjwa hao.

Vile vile Mratibu wa Kampeni ya Kemikali za Trans-fat Tanzania, Yosia Kimweli, anasema trans-fat, ina madhara kifya uthibitisho uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na wanasayansi, kuwa inasababisha magonjwa ya moyo pamoja na mishipa ya damu.

Mfano wa vyakula hivyo keki, vidakuzi, mikate, bisibisi, pizza iliyogandishwa, biskuti, donati na kuku wa kukaanga, watu walio wengi wamejikuta wakitumia vitu hivyo ikiwa hawafahamu madhara ya kiafya kwa siku za mbeleni.

WHO inaishauri kiwango cha kemikali ya 'transfat' kiwe asilimia mbili, kwani kiwango zaidi ya hiyo kinasababisha hayo magonjwa, hivyo inahitajika kutungwa sheria kwa nchi za umoja wa mataifa kwani ni baadhi ambazo tayari zimeshatunga sheria kwa Afrika ni nchi mbili, za Afrika Kusini na Nigeria pekee.

Anasema kwa upende wa nchi za Afrika masahariki huna ambayo tayari imetunga sheria, ili kupunguza kiwango cha matumizi ya transfat kwenye bidhaa na kupunguza madhara hayo nchini.

Hivyo wakiwa kama Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania, wanaiyomba selikari itunge sheria ya trans-fat, ili kulinda afya za watanzania pia kuendana na nchi wanachama wa umoja wa mataifa udhibiti majanga hayo nchini.

Lebo zenye kuonekana zitafanya mlaji kuwa na maamuzi sahihi, katika kuchagua chakula chenye kujenga mwili kiafya na hata kuepuka magonjwa yasiyoambukiza, ambayo husababishwa na vyakula hivyo.

### SHERIA YENYEWE

Sheria ya Usalama wa Bidhaa za Watumiaji (CPSA), inasema lebo ya ufuatiliaji inapaswa kujumuisha mtengenezaji na mnunuzi, maelezo kama vile mahali na tarehe ya utengenezaji wa bidhaa, bechi, nambari ya uendeshaji au sifa zingine tambulishi na maelezo mengine yaliyoamuliwa na mtengenezaji, ili kusaidia kutambua chanzo mahususi cha bidhaa.

Taarifa zote za lebo ya ufuatiliaji lazima zionekane na kusomeka Kiambato kinapotambuliwa kuwa hatari au chanzo cha ukiukaji, lebo ya ufuatiliaji husaidia kutambua bidhaa zingine zilizo na kiungo sawa.

Sheria husika imo katika kifungu cha 14(a)(5) cha Sheria ya Usalama wa Bidhaa za Mtumiaji (CPSA), masharti haya hapo awali yalikuwa sehemu ya kifungu cha 103 cha Sheria ya Uboreshaji wa Usalama wa Bidhaa za Mtumiaji (CPSIA).

## Mageuzi bei korosho yalivyomletea uhai mkulima, hadi bandari Mtwara

INATOKA UK.11

### WAZIRI KILIMO

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anaeleza kuwa serikali inakusudia kujenga kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kuhudumia tani 3,000 kwa mara moja, pamoja na kujenga maghala mawili yatakayohifadhi tani 10,000 kila moja.

Bashe akasisitiza :"Ruzuku za dawa za maji na 'sulphur' zitaendelea kutolewa bure kwa wakulima wa korosho."

Anaitaja kuwa hatua muhimu katika kuhakikisha wakulima wanapata msaada unaohitajika ili kuboresha uzalishaji wao.

Kimsingi, uzalishaji korosho ambao unashika Uchumi wa umma, unatoa fursa ya kuboresha maisha ya wakulima na jamii nzima

Hapo inabeba tafsiri kwamba, soko la korosho linaweza kuwa msingi wa ukuaji wa uchumi wa mikoa ya Mtwara na Lindi, kila mzalishaji anapaswa kuchangia ufanisi katika mchakato mzima kuhuisha ao hiloio sokoni.



MLIPUKO WA KIPINDUPINDU

# DC asitisha shughuli za uvuvi

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MKUU wa Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, Thomas Apson, ameagiza kufungwa bwawa la uvuvi samaki la Wembere lililoko Kata ya Mgungira kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu kwenye eneo hilo.

Apson alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha wataalamu wa afya ambacho pamoja na mambo mengine kilijadili mlipuko huo katika kijiji cha Ufana na maeneo yanayozunguka bwawa la Wembere.

Mkuu huyo ambaye hata hivyo hakutaja idadi ya watu waliougua ugonjwa huo hadi sasa, alisema timu ya watoa huduma za afya inaendelea kutoa matibabu kwa waliougua ugonjwa huo katika kambi maalumu zilizotengwa.

Alitoa wito kwa wananchi kutumia maji safi na salama majumbani, kunawa kwa maji tiririka kwa sabuni wanapotoka msalani ili kuzuia maambukizi zaidi ya ugonjwa huo.

**Alitoa wito kwa wananchi kutumia maji safi na salama majumbani, kunawa kwa maji tiririka kwa sabuni wanapotoka msalani ili kuzuia maambukizi zaidi ya ugonjwa huo.**

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Ludovick na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Justice Kijazi, walisema kuwa kuzuia maambukizi zaidi ya ugonjwa huo, hakuna budi kuchimbwe visima vya maji safi na salama na kujenga vyoo bora katika vijiji vya kata hizo.

Wataalamu wa afya waliomba serikali kuongeza dawa, vifaa tiba, vitendanishi na mahitaji mengine muhimu katika kambi za kipindupindu.

Agosti mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliwaagiza maofisa afya mkoani mwake kuwachukulia hatua kali wananchi ambao watabainika kukaidi kufanya usafi katika maeneo yao kama hatua ya kuondoa tatizo la magonjwa ya mlipuko, kikiwamo kipindupindu.




Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mtafiti wa mradi wa Kilimo na Data, Dk. Godfrey Justo, akifafanua jambo wakati wa uzinduzi wa mradi huo, jijini Dodoma jana, utakaotekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Manyara na Pemba kwa muda wa miaka miwili ukiwa na lengo la kufundisha umuhimu wa matumizi ya taarifa za hali ya hewa, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima vijana na wanawake. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wafanyakazi waonywa rushwa, matumizi mabaya ya madaraka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi amewataka wafanyakazi wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) kuzingatia maadili na miiko ya kazi wawapo kazini ili kujiepusha na vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.

Godfrey Kasekenya alitoa angalizo hilo jana na jijini hapa wakati wa uzinduzi wa baraza hilo lilolo chini ya wizara hiyo.

"Niwaonye msifuge ubovu katika taasisi kwa kuwalinda na kuwatetea watumishi wazembe wanaokwenda kinyume kwa kukiuka taratibu za kazi, kufanya hivyo wanawakatisha tamaa watumishi wanaojituma na kutekeleza majukumu yao ipasavyo," alisema.

Kasekenya alisema Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu mahala pa kazi, hivyo wanapaswa kulitumia kujadili changamoto mbalimbali zinazowahusu, ikiwamo bajeti ya serikali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Alisema kuwapo Baraza la Wafanyakazi kunatoa fursa kwa watumishi kujadili masuala ya msingi ya taasisi, ikiwamo mipango, bajeti na masuala mengine ya kiutendaji ili kuyafikia malengo ya taasisi hiyo.

Naibu Waziri Kasekenya pia aliwapongeza NCC kutokana na kutekeleza agizo la Waziri wa Ujenzi la kuanzisha Baraza la Wafanyakazi ambalo ni chombo cha kutatua migogoro baina ya watumishi inayochangia kudhoofisha utendaji wa kazi.

"Nawapongeza kuanzisha Baraza la Wafanyakazi, lakini liende kutumika katika misingi inayotakiwa kwenye utendaji kazi za kila siku," aliagiza Kasekenya.

Mbali na hayo, alisisitiza watumishi hao kujitokeza kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao ni haki ya kila mmoja kujiandikisha kupiga kura ili kuchagua viongozi sahihi wanaoleta maendeleo katika taifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya NCC, Dk. Fatuma Mohamed, alisema NCC imejipanga kushirikiana na baraza hilo katika utendaji wa majukumu yao ili kufikia malengo yao.

Awali, Mkurugenzi wa Utawala wa wizara hiyo, Mrisho Mrisho, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, alisema kuwapo kwa baraza hilo kutawezesha urahisi wa utendaji kazi zao za kila siku na kuwahimiza watumishi kufanya kazi kwa umoja na mshikamano.

# Mhadhiri ataka wakulima watumie taarifa za TMA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Saalam (UDSM) na Mtafiti wa Mradi wa Kilimo na Data, amewashauri wakulima kutumia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi ili kuongeza tija kwenye kilimo na kuondokana na kilimo cha mazoea. Dk. Godfrey Justo alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wakati wa uzinduzi wa mradi huo.

Alisema kuwa hivi sasa wakulima wengi wanalima kwa mazoea na kukariri msimu wa kilimo bila kupata taarifa sahihi za mamlaka ambazo zitawawezesha kujua msimu unaanza mwezi gani, pia kiwango cha mvua.

"Wakulima wengi wanalima kwa mazoea. Kama watawezesha kupata taarifa sahihi za hali ya hewa wataweza kulima kwa tija kwani watajua kiwango cha mvua katika msimu husika na kama kutakuwa na ukame watajipanga kupata mbegu ambazo zitakabiliana na ukame," alisema.

Aliongeza kuwa mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yanabadili misimu na kiwango cha mvua kwa kunyesha juu ya wastani au chini ya wastani, hivyo kuwapo taarifa za hali ya hewa ni muhimu kwa wakulima ili wajiandae kukabiliana na hali hiyo.

Kuhusu mradi, Dk. Justo alisema utatekelezwa kwa muda wa miaka miwili na Shirika la Tanzania Data Lab (d LAB) katika mikoa ya Dodoma, Manyara pamoja na Pemba, walengwa ni vijana na wanawake.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwezesha wakulima vijana na wanawake ambao wamekuwa wakijihusisha na kilimo cha mazao ya biashara kutumia taarifa sahihi za hali ya hewa ili kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi.

"Lengo la mradi huu ni kuwawawezesha wakulima ambao wanalima mazao ya biashara kutumia taarifa sahihi za hali ya hewa ili kuondokana na kilimo cha mazoea na kuongeza tija kwenye kilimo na kujiongezea kipato," alisema. Alisema mradi huo utahusisha vijana na wanawake kutokana na makundi hayo kuwa katika hatari zaidi ya mabadiliko tabianchi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Sekta za Uchumi na Uzalishaji Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Enock Nyanda, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuweka mazingira rafiki kwa wakulima. "Tunawashuru d LAB kwa kuleta mradi huu ambao utakwenda kusaidia wakulima vijana na wanawake kupata taarifa za hali ya hewa ili kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi lakini pia utakwenda kusaidia changamoto ya ajira kwa makundi haya," alisema. Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la COSITA Tanzania la mkoani Manyara, Patrice Gwasma, alisema mradi huo utakuwa msaada mkubwa kwa wakulima ambao wamekuwa wakikabiliwa na athari za mabadiliko tabianchi kwa muda mrefu.





# Majeruhi 1,200 ajali miezi sita watibiwa hospitali rufani kanda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya majeruhi 1,200 wa ajali za barabarani wamepokewa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya katika kipindi cha miezi sita, takwimu ambazo zimeushtua uongozi wa hospitali hiyo na kusema ni kubwa.

Mkuu wa Kitengo cha Mifupa na Majeraha wa Hospitali hiyo, Dk. John Mbaga, alisema jana kuwa kiwango hicho ni sawa na asilimia 90 ya majeruhi wote waliofikishwa hospitalini hapo kupata matibabu.

Alisema idadi hiyo ya majeruhi wanaotokana na ajali za barabarani ni kubwa na kwamba kuna haja ya kutafuta njia za kupunguza ajali za barabarani.

Dk. Mbaga pia alisema majeruhi wanaotokana na pikipiki maarufu kwa jina la bodaboda ndio wengi wakifuatiwa na vyombo vingine vya moto kama vile magari na bajaj.

"Sisi kama hospitali tumeona idadi ya majeruhi wa ajali wanaoletwa kwa ajili ya matibabu ni kubwa na hatuwezi kuacha hali iendelee hivi.

Ni lazima tushirikishe wadau wengine ili kuona namna ya kupunguza ajali hizi ambazo ni chanzo kikubwa cha majeruhi wanaofika katika hospitali yetu," alisema Dk. Mbaga.

**Alisema katika kushirikisha wadau, hospitali imeamua kuandaa mdahalo maalum wa kujadili namna ya kupunguza ajali hizo utakaofanyika jijini Mbeya.**

Alisema katika kuwashirikisha wadau, hospitali imeamua kuandaa mdahalo maalum wa kujadili namna ya kupunguza ajali hizo utakaofanyika jijini Mbeya.

Mratibu wa mdahalo huo ambao umeandaliwa na hospitali kwa kushirikiana na Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Gidion Makulila, alisema utashirikisha wadau wote wa usalama barabarani.

Alisema lengo ni kutafuta mbinu za kupunguza au kumaliza kabisa ajali za barabarani mkoani Mbeya.

Alisema miongoni mwa wadau watakaoshiriki mdahalo huo ni Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), madereva wa bodaboda, madereva wa magari na watumiaji wengine wa barabara.

"Tunahitaji wadau wote hawa tukae pamoja tujadili namna ya kupunguza ajali mkoani Mbeya ili tuepushe majeruhi ambao wamekuwa wakiongezeka kila mwaka," alisema.

Katibu wa Kamati ya Maandalizi ya Mdahalo huo, Joyce Komba, alisema ajali za barabarani zimekuwa na madhara makubwa kwenye jamii hivyo ni muhimu kutafuta mbinu za kupunguza ajali hizo ili kuepusha madhara hayo kwenye jamii.

Alisema mbali na ajali kusababisha majeruhi, baadhi ya watu wanapata ulemavu wa kudumu, wengine wanakufa na kuacha familia zikitaabika huku serikali nayo ikiathirika kwa kutumia fedha nyingi kuagiza dawa kwa ajili ya matibabu ya watu wanaoumia ajalini.

Mdahalo huo umepangwa kufanyika wiki hii jijini Mbeya ili wadau wa usalama barabarani watumie fursa hiyo kujadili na kuweka mikakati thabiti ya kupunguza ajali mkoani Mbeya.



Mmoja wa viongozi wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Memune Kinana (kulia), akitoa maoni kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa mifugo hifadhini, wakati wa kikao na viongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wilayani humo, mkoani Mbeya, hivi karibuni **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bil. 133/- kuboresha sekta ya fedha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 133 kwa ajili ya kuboresha sekta ya fedha ikiwamo kutengeneza mikakati ya kuwafanya wananchi waondokane na matumizi ya mifumo isiyo rasmi ya fedha.

Fedha hizo zitatumika kufanya utafiti kwenye sekta ya fedha, kutoa elimu ya matumizi ya huduma rasmi za fedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati pamoja na kuongeza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye sekta ya fedha.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipomwakilisha Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwenye ufunguzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha ambayo kitaifa yanafanyika jijini Mbeya.

Alisema fedha hizo zilianza kutumika katika mwaka wa fedha 2021/22 na matumizi yake yatafikia ukomo mwaka 2025/26 na kwamba matumizi hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa tatu wa maendeleo ya taifa.

"Lakini pia serikali inaendelea na mchakato wa maboresho ya mtaala mpya wa elimu ambao unalenga kuingiza elimu ya fedha na ujasiriamali kwa vijana wetu ili kila mmoja awe na uwezo wa kujiajiri. Mchakato huu utakapokamilika tutawajulisha wadau," alisema Prof. Mkenda.

Mwakilishi wa Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia huduma rasmi za fedha ifikapo mwaka 2026.

Alisema maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha yanafanyika kwa lengo la kufikisha elimu kwa wananchi kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu sekta ya fedha ikiwamo matumizi sahihi ya mifumo ya fedha ili kukuza uchumi.

Alisema kwa sasa asilimia 46 ya Watanzania bado wanatumia huduma zisizo rasmi za fedha ikiwa ni pamoja na kuhifadhi ndani ya nyuma, kuweka kwenye vibubu na wengine kufukia.

"Wadau wote waliopo kwenye maadhimisho haya wanatoa elimu ya matumizi ya huduma rasmi za fedha, katika kipindi cha wiki nzima elimu hii itatolewa hapa," alisema Dk. Mwamwaja.

Baadhi ya wadau walioshiriki kwenye maadhimisho hayo walisema watayatumia maadhimisho hayo kuwahamasisha wananchi kutumia huduma rasmi za fedha hasa kwa wananchi wa maeneo ya vijijini.

Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Mwanjelwa jijini Mbeya, Khalid Omary, alisema benki hiyo inaendelea kuboresha huduma kwa kufungua matawi mapya vijijini, kuanzisha mifumo ya Tehama na kuanzisha mawakala katika maeneo mbalimbali ya vijijini ili kuwasaidia wananchi.

# Waonywa uuzaji wa mbolea feki

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

KAMPUNI za pembejeo za kilimo mkoani Njombe zimeonywa kutojihusisha na kuuza mbolea, mbegu na viuatilifu feki kwa maelezo kuwa zitachukuliwa hatua kali za kisheria.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, wakati akizindua msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2024/25 katika Kijiji cha Ilembula wilayani Wanging'ombe mkoani hapa.

Mtaka alisema katika msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24, wakulima walipata hasara kutokana na kuuziwa pembejeo feki na baadhi ya kampuni.

"Tuna uzoefu msimu kama huu wa kilimo watu kutumia fursa. Niwaombe wananchi wa Mkoa wa Njombe hatutakuwa na msamaha kwa mtu tutakayemkamata akiwa anauza pembejeo feki za kilimo kwa sababu vyombo vya sheria vitachukuwa mkondo wake, hivyo tusije tukalaumiana," alisema.

Mtaka aliwataka wananchi kushirikiana na serikali ili kuwabaini wafanyabiashara ambao wanauza bidhaa bandia za pembejeo.

"Naomba wananchi waende kununua kwenye vituo ambavyo tunavitangaza kwa ajili ya kununua mahitaji ya pembejeo lakini wananchi pia wawe na waangalifu na wawe masikio yetu ya kuwabaini wale watu ambao wanauza bidhaa bandia pamoja na kuchukuwa tahadhari na kuona kwamba hii sio bidhaa ya kuchangamkia," alisema Mtaka.

Ofisa Kilimo Mkoa wa Njombe, Wilson Joel, alisema lengo la uzinduzi huo ni kuwafikishia wakulima pembejeo katika maeneo yao kwa sababu tayari serikali imeweka ruzuku kwenye mbolea na mbegu.

"Mara nyingi kumekuwa na changamoto ya ufikaji wa hizi pembejeo kwa wakulima kulingana na miundombinu, geografia, uchache wa mawakala lakini pia na watumishi wachache wa makampuni," alisema.

Joel pia alisema wakulima katika vituo hivyo watapata elimu kwa sababu ya uwapo wa matukio ya wakulima kudanyanywa kuhusu pembejeo feki.

Naye Bwana Shamba kutoka kampuni ya Mtewele General Traders, Musa Lwinga, alisema wamejipanga kuhakikisha wanatoa elimu kwa wakulima pamoja na kuwafikishia pembejeo kwa wakati katika maeneo yao.

Mmoja wa wakulima katika kijiji cha Ilembula, Veronica Mtweve, aliomba serikali msimu huu wa kilimo kusimamia kampuni ili zisiwauzie pembejeo feki ambazo ziliwasababishia hasara kutokana na mazao kuharibika shambani.



## HABARI ZANZIBAR

# Kasi magonjwa yasiyoambukiza yatisha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HALI ya magonjwa yasiyoambukiza imeendelea kuwa tishio kwa ustawi wa wanadamu duniani kote na kwa Zanzibar, yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka.

Ongezeko hilo limesababisha vifo vingi na kuacha ulemavu ikiwa ni pamoja na kuongeza utegemezi wa wagonjwa kwa familia kutokana na kuugua kwa muda mrefu.

Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya wa Wizara ya Afya, Dk. Salim Slim, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini hapa, kuhusu kilele cha Wiki ya Maradhi Yasioambukiza Duniani.

Dk. Slim alisema katika maadhimisho hayo watu 968, wakiwamo wanawake 637 na wanaume 331 Unguja na Pemba, wamepimwa afya zao kwa kuangalia hali za lishe, uwiano wa uzito na urefu (BMI), vipimo vya kisukari na shinikizo la damu.

Alisema takwimu zinaonyesha watu 19 sawa na asilimia mbili waliopimwa walithibitika kuugua maradhi ya kisukari sawa na asilimia 26 walithibitika kuwa na maradhi ya shinikizo la juu la damu.

"Hii inathibitisha hali halisi ya maradhi yasioambukiza na uwapo wa haja ya kushirikiana kuongeza juhudi katika mapambano ya maradhi haya nchini mwetu," alisema.

**"Hii inathibitisha hali halisi ya maradhi yasioambukiza na uwapo wa haja ya kushirikiana kuongeza juhudi katika mapambano ya maradhi haya nchini mwetu," alisema.**

Pia alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekeza nguvu nyingi katika kupambana na maradhi hayo na uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar ni sehemu ya juhudi za mapambano hayo.

"Ieleweke kuwa matibabu ya maradhi yasioambukiza yanatumia gharama kubwa na kuathiri hali ya kiuchumi ya mtu mmoja mmoja, familia na taifa kwa ujumla," alisema.

Hata hivyo, alisema takwimu za gharama za maradhi ya kisukari na shinikizo la damu kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) zinaonesha ongezeko lisilo la kawaida na kugharimu fedha nyingi za mfuko.

Alisema kwa mfano, mwaka 2016/17 idadi ya wagonjwa wa figo waliokuwa wakihudumiwa na NHIF walikuwa 280 wakati mwaka 2021/22 waliongezeka hadi kufikia 2,099.

Pia alisema gharama za matibabu kwa magonjwa yasiyoambukiza zilizokuwa zikilipiwa na NHIF kwa mwaka 2016/17 zilikuwa Sh. bilioni 35.65 na mwaka 2021/22 zilizongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 99.09.

"Hii inaonesha ni kwa kiasi gani ongezeko la maradhi yasioambukiza yanavyoathiri maendeleo yetu kiafya, kijamii na kiuchumi," alisema.

Kutokana na ongezeko hilo, aliitaka jamii kujitahidi kula mlo bora na unaofaa na kuushughulisha mwili kwa namna mbalimbali ikiwamo kufanya mazoezi, kuachana na vichocheo vyote vya maradhi yasiyoambukiza ili kuendelea kuishi wakiwa wenye afya na kujenga taifa.



Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Salim Slim, akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu wiki ya magonjwa yasiyoambukiza. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mahujaji 3,600 Tanzania kuhiji Macca mwaka 2024

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAHUJAJI 3,600 wanatarajiwa kwenda kuhiji Makkah nchini Saudi Arabia kwa mwaka 1446 Hijiria sawa na mwaka 2025.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Taasisi za Umoja wa Hijja Tanzania, Sheikh Ali Adam Ali, alibainisha hayo jana mbele ya waandishi wa habari katika Masjidi Zinjibar, visiwani hapa.

Alisema licha ya serikali ya Saudi Arabia kutoa nafasi 25,000 kwa mahujaji wa Tanzania, bado idadi yao haijafika hata robo inayotakiwa.

Sheikh Ali alisema ikiwa mwaka huu wa maandalizi ya Hijja yanaanza mapema, mwavuli wa taasisi hizo unakaridia kuwapeleka mahujaji kiwango hicho cha watu 3,600 kwa Tanzania nzima ambao kwa Zanzibar watakuwa 2,300 huku Tanzania Bara 1,300.

"Taasisi yetu imejipanga kuhakikisha mahujaji kwa Zanzibar na Tanzania Bara kuwa wanakwenda kwenye ibada hiyo bila wasiwasi wowote na tuko tayari kwa hilo," alisema.

Alisema kwa muda mrefu serikali ya Saudi Arabia ilitoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa ibada ya hijja, kutokana na mpango wake wa muda mrefu wa maendeleo.

Mwenyekiti huo alisema kuwa serikali hiyo imeyapa kipaumbele mambo mbalimbali katika utekelezaji wa ibada hiyo ili kuondosha changamoto zinazowakabili mahujaji.

Pia alisema serikali ya Saudi Arabia kupitia wizara inayohusiana na masuala ya hijja na umrah imetoa ratiba mpya ya miongozo ya utekelezaji wa ibada ya hijja baada ya kukamilika kwa ibada ya mwaka 2024.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Hijja na Umra na Ziara kutoka Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar, Hassan Rashid Mohmmed, alisema lengo la kuwapo kwa mfuko wa hijja ni kutoa nafasi kwa wananchi kuweka pesa zao ili kwenda Makkah kuhiji .

# Wenye ulemavu wasisitizwa kushiriki uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Ussi Khamis Debe, amewataka watu wa kundi hilo kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Ili kushiriki katika uchaguzi huo, wamesisitizwa kuhakiki taarifa zao katika daftari la kudumu la wapigakura, kwa sababu ni moja ya haki zao za msingi.

Ussi aliyasema hayo visiwani hapa wakati akimwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Suleiman, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani, ambayo kilele chake ni Novemba 3, kila mwaka. Kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yatafanyika kisiwani Pemba.

Aliwataka wale ambao hawajajiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura wajitokeze kufanya hivyo ili kupata fursa katika uchaguzi mkuu kuwachagua viongozi ambao wataleta mapinduzi makubwa katika kuijenga Zanzibar kwenye sekta za kiuchumi na kijamii.

Ussi alisema ni vyema kwa watu wenye ulemavu kuwa na uthubutu katika kugombea nafasi mbalimbali za kiuongozi, kuanzia wadi hadi taifa.

"Ni matumaini yangu kuwa wako watu wenye ulemavu wana uwezo wa kushiriki katika uchaguzi. Sambamba na hilo, naomba pia watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi katika kushiriki kuwachagua viongozi wetu," alisema.

Pia alisema historia inaonesha kwamba harakati za kupigania haki na fursa za watu wenye ulemavu zilianza miaka ya 1970 kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa baada ya kupitia na kuangalia masuala yote yanayohusu maisha na maendeleo ya watu wote duniani.

Alisema imeonekana kuwa bado masuala ya watu wenye ulemavu hayajatiliwa mkazo wa kutosha hasa katika upande wa suala la haki za kibinadamu.

Alisema hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa miaka mingi kuanzia mwaka 1981 hadi 1992 na uamuzi wa mwisho ulitangazwa Desemba 3, 1992 kuwa kila ifikapo siku hiyo ni kutakuwa na Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani kwa misingi ya kuhakikisha suala la watu hao ni moja ya masuala ya haki za binadamu.

"Ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanamudu maisha yao, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelipa kipaumbele suala la haki za watu wenye ulemavu kwa kuanza kuchukua hatua za makusudi ili kufikia kuwa na jamii jumuishi," alisema.

Alizitaja hatua hizo ni pamoja na kutungwa kwa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayosimamia haki za watu wenye ulemavu, kuundwa kwa Baraza la Taifa na mabaraza ya wilaya ya watu wenye ulemavu na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu ambapo tayari umeanza kufanya kazi za kuwahudumia watu wa kundi hilo.

Pia alisema hatua nyingine ni kuendelea kusimamia upatikanaji wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu kwa kuanza kukagua majengo mbalimbali ya umma na binafsi na serikali imejenga shule mbili mahususi kwa ajili ya watu wenye ulemavu Jendele na Pujini.

"Serikali imetenga fedha kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zinazotokana na makusanyo ya halmashauri," alisema. Naye Ofisa Utawala wa Taasisi ya Zanzibar Initiative Organization, Twalaa Juma Khamis, alisema waandishi wa habari wana mchango mkubwa katika kuelimisha jamii kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu.

Alisema katika kuelekea maadhimisho hayo, taasisi hiyo itashiriki kikamilifu kuanzia programu zote ambazo zimeandaliwa ili kuwahamasisha watu wenye ulemavu kupitia shughuli wanazozifanya.

# Ufaransa kuisaidia Lebanon bil. 1.5/-

**PARIS,** Ufaransa

UFARANSA imekusanya kiasi cha dola milioni 540 (Sh. bilioni 1.5) kwa ajili ya kuisaidia Lebanon ambayo siku chache zilizopita iliingia kwenye machafuko na Israel baada ya kuingilia kati vita vya ukanda wa Gaza.

Waraka uliotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa ulisema fedha hizo zilikusanywa katika mkutano uliofanyika jana ambako uliwakutanisha wajumbe 70 na ulilenga kuibua mikakati madhubuti kwa ajili ya kuisaidia Lebanon.

Kwa mujibu wa waraka huo, msaada huo kimsingi utalenga kutoa huduma za kijamii kama afya, chakula, maji, usafi hadi elimu kwa watu walioyakimbia makazi yao.

Wakati huo huo, Lebanon ilisema inahitaji dola milioni 250 sawa na Sh. bilioni 681kwa mwezi kwa ajili ya kukabiliana na mzozo uliosababisha kati ya watu 500,000 hadi milioni 1 kukimbia kutoka kusini mwa nchi hiyo tangu Israel ilipoanza kulishambulia kundi la Hezbollah mwezi Septemba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa mamlaka ya Lebanon, mashambulizi hayo yamesababisha vifo vya zaidi ya raia 2,000 na wengine zaidi ya milioni moja kuyahama makazi yao.

Ufaransa inatumai kuwa uhusiano wake wa karibu wa kihistoria na Lebanon unaweza kusaidia kuleta suluhu si tu ya usitishaji wa mapigano, bali pia wa muda mrefu kwenye eneo hilo.

Kabla ya mkutano huu wa kimataifa wa misaada uliofanyika mjini Paris, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema anataka kutoa misaada ya kibinadamu, kuunga mkono jumuiya ya kimataifa na vikosi vya jeshi la Lebanon kuimarisha usalama, hasa kusini mwa nchi hiyo.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa ilisema inatarajia wawakilishi kutoka mataifa washirika wa Lebanon, Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Ulaya (EU) na mashirika mengine ya kimataifa, kitaifa, kikanda, na kiraia yataunga mkono uhuru wa Lebanon.

Mwenyekiti wa idara ya historia mamboleo katika ulimwengu wa Kiarabu kwenye Chuo cha Ufaransa huko Paris, Henry Laurens alisema taifa hilo na Lebanon lina uhusiano wa kina wa kisiasa na kitamaduni.

Alisema serikali ya Ufaransa ilikuwa na jukumu muhimu la kidiplomasia hapo awali kwa sababu ilizungumza na pande zote hasa kutokana na historia yake ya ukoloni.

"Tangu katikati ya karne ya 19, shirika la hisani la Ufaransa 'L'Oeuvre d'Orient' limekusanya fedha kwa ajili ya mashirika ya elimu, matibabu na kidini, hasa nchini Lebanon," alisema, akiongeza kuwa Lebanon pia ilikuwa chini ya uangalizi wa Ufaransa kuanzia 1920 hadi 1943.

Macron alitoa wito wa kukomeshwa upelekwaji silaha nchini Israel na kusisitiza haja ya suluhisho la kisiasa, hata katika vita vya huko Gaza. Na kwamba hiyo ilichochea hasira ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, ambaye aliyaita maneno ya aibu.**DW**

## Tshisekedi ataka katiba irekebishwe

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Félix Tshisekedi, amesema kuwa katiba ya nchi hiyo inapaswa kurekebishwa kwa sababu ina udhaifu fulani, licha ya kwamba idadi ya mihula ya urais haitabadilishwa, huku wapinzani wakisema anania ya kuwania muhula wa tatu.

Ilielezwa kuwa ni mara ya kwanza kwa Rais Tshisekedi kuzungumza hadharani kuhusu suala hilo lenye utata, baada ya chama chake cha UDPS kuanzisha kampeni mwezi huu ya kurekebisha katiba.

Katika hotuba aliyoitoa jana nchini humo Rais Tshisekedi, alisema kuwa katiba inapaswa kurekebishwa kulingana na hali halisi ya Kongo.

Pia kiongozi huyo alisema kuwa hatua hii haitaathiri idadi ya mihula katika uchaguzi wa rais lakini wapinzani wake wanasema kuwa ni njia ya kujaribu kufanya kampeni kwa ajili ya muhula wa tatu.

Ilielezwa kuwa wapinzani nchini DRC wanamshinikiza kiongozi huyo aachie madaraka wakati muhula wake wa pili alioapishwa Januari 1, mwaka huu utakapomalizika.

Aidha, ilibainishwa kuwa miongoni mwa sababu alizozitoa, Tshisekedi alieleza kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kuanzisha taasisi baada ya uchaguzi wa hivi karibuni, na kwamba kuna udhaifu katika mamlaka ya wakuu wa mikoa. **BBC**







Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, akimsikiliza Waziri Mkuu wa Lebanon, Najib Mikati (kushoto), wakati wa mkutano wa kimataifa kuhusu Lebanon mjini Paris, jana. **PICHA: AP**

## Jumuiya ya Madola waikaidi Uingereza

**LONDON,** Uingereza

WAKUU wa serikali za Jumuiya ya Madola wanajiandaa kuikaidi Uingereza na kukubaliana kuhusu mipango ya kuchunguza haki ya malipo ya biashara ya utumwa iliyovuka Bahari ya Atlantiki.

Hayo yamejiri baada ya Waziri Mkuu Sir Keir Starmer (pichani) kusema kwamba anataka kujadili changamoto za sasa na viongozi wa Jumuiya ya Madola, kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa, badala ya siku zilizopita.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Downing Street ilisisitiza kuwa suala hilo haliko katika ajenda ya mkutano wa kilele wa nchi 56 za Jumuiya ya Madola, ambao utaanza katika kisiwa cha Samoa kwenye kisiwa cha Pasifiki leo.

Vyanzo vya kidiplomasia vilisema maofisa walikuwa wakijadili makubaliano ya kufanya utafiti zaidi na kuanza mazungumzo ya maana kuhusu suala ambalo linaweza kuiacha Uingereza ikidaiwa mabilioni ya pauni za fidia.



Ilielezwa kuwa haki ya urejeshaji wa utumwa inaweza kuja kwa njia nyingi, ikiwa ni pamoja na fidia ya fedha, msamaha wa deni, kuomba msamaha rasmi, programu za elimu, ujenzi wa makumbusho, msaada wa kiuchumi, na usaidizi wa afya ya umma.

Aidha, ilielezwa kuwa Uingereza haikutaka lugha yoyote katika tamko kuhusu haki ya upatanishi, lakini kwa sasa inabidi ikubali itajumuisha aya tatu kamili zinazoelezea msimamo wa Jumuiya ya Madola.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa maofisa kutoka Caricom, chombo kinachowakilisha nchi za Carribean wametaka kupanua suala hili ili lijumuishe sio biashara ya watumwa tu katika Atlantiki bali pia Pasifiki.

Tamko la rasimu lilisema nchi nyingi wanachama zinashiriki uzoefu wa kawaida wa kihistoria kuhusiana na biashara hii ya kuchukiza, na kunyang'anywa mali kwa watu wa asili. **BBC**

# MGUNDA ATUA NAMUNGO, NYOTA 'WALIA' LIGI NGUMU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikimtangaza rasmi, Juma Mgunda, kuwa kocha mpya wa Namungo FC, wachezaji wa timu hiyo wamesema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ni ngumu zaidi kuliko misimu iliyotanguliwa ambayo wameshiriki.

**Namungo leo watakuwa ugenini dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.**

Wachezaji wa timu hiyo, Frank Domayo, Hassan Kabunda na Paul Buswita, kwa nyakati tofauti wamebainisha ligi imekuwa ngumu kwa sababu mbalimbali, ikiwamo klabu kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa na uzoefu.

"Ligi ya mwaka huu kiboko, ni ngumu sana, unajua mimi ni mzoefu wa ligi ya Tanzania, huwa inaanza taratibu sana na mechi zinakuwa laini mpaka mzunguko wa pili ndiyo timu zinakaza, haianzi kwa ushindani kama huu tunaouona sasa, safari hii imekuja kivingine.

Mzunguko huu wa kwanza tu unaona kabisa imekuwa ngumu mno na kila timu imejipanga kuhakikisha inafanya vizuri na unaona timu inashinda popote, nyumbani ugenini, huwezi kusema kwa sababu upo nyumbani utashinda kirahisi," alisema Domayo, kiungo huyo wa zamani wa Yanga na Azam FC.

Kwa upande wake, winga, Buswita, alisema hata wao Namungo wanasuasua si kwa sababu wana timu mbaya, ila ni ushindani uliopo kwa sasa katika ligi hiyo.

"Sisi Namungo tuna malengo, lakini hatujayafikia mpaka sasa kwa sababu timu nyingi zimejiandaa, ligi yetu imekua sana tofauti na miaka ya nyuma, miaka ya sasa kila timu inaweza kusajili mchezaji yoyote kutoka popote, kwa maana hiyo wanakuja wachezaji wenye viwango vikubwa sana nchini na wenye uzoefu, " alisema nyota huyo wa zamani wa Yanga.

Naye Hassan Kabunda, alisema siku hizi kila wanapokwenda kucheza mechi ya Ligi Kuu ni kama wanakwenda kucheza mchezo wa fainali, tofauti na zamani.

Kabunda alisema misimu iliyotangulia michezo yenye ushindani na migumu ilikuwa michache lakini kwa sasa hakuna mechi rahisi.

"Ligi ni ngumu kweli kweli, yaani siku hizi kila mechi mnakwenda kucheza inakuwa kama fainali, hakuna kusema ukicheza na Simba, Yanga, Azam ndiyo inakuwa ngumu, hata ukicheza na timu ya kawaida, mtakachokikuta uwanjani ni bora mcheze na timu hizo kubwa, na nadhani huko mbele ya safari itazidi kuwa ngumu zaidi," alisema Kabunda.

Mgunda ametua katika kikosi hicho akichukua mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera ambaye kwa sasa atatambulika kama mshauri wa benchi la ufundi.

Baada ya mechi ya Simba, Namungo itarejea nyumbani kwenye Uwanja wa Majaliwa kuwasubiri Pamba Jiji katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Oktoba 28, mwaka huu.



Mchezaji wa Timu ya Vijana JMK Park, Shaban Ramadhan (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Mzambarauni, Issa Ali, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa kituo hicho Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *TPA, NSSF kupamba michuano ya ngarawa*

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Resi za Ngarawa Salama kwa Uvuvi Endelevu Tanzania yanatarajia kufanyika Novemba 3, mwaka huu kwa ajili ya kuadhimisha miaka minne ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, imeelezwa.

Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), wamethibitisha kudhamini mashindano hayo.

Mratibu wa mashindano hayo, Abdallah Majura, alisema mashindano hayo yatafanyika kuanzia Soko la Wavuvi Fumba kuelekea Kisiwa cha Pungume na kurudi Fumba na yatakuwa na umbali wa kilomita 27.

Majura ameziomba taasisi nyingine kujitokeza kusaidia mashindano hayo ili yafanyike kwa ufanisi mkubwa na kutoa zawadi kwa washindi.

"Lengo letu ni kushirikisha ngarawa 100 ambazo tungezigawa kwenye makundi matano ambapo kila kundi litakuwa na ngarawa 20, lakini tunapata mashaka huenda lengo lisifikiwe kwa sababu baadhi ya taasisi tulizozienda hazikutoa ushirikiano tuliotarajia.

Tunataka waendesha ngarawa watakaoshiriki kufichua vitendo viovu vinavyofanyika baharini mfano uvushaji wa bidhaa kwa njia ya magendo kupitia baharini kutoka pande zote za Muungano," alisema Majura.

Aliongeza waendesha ngarawa hao wanatarajiwa kuwa mabalozi wazuri wa kufichua uvuvi haramu mfano wa kutumia zana ambazo zinaharibu mazalia ya samaki au vifaa visivyoruhusiwa kufanyiwa uvuvi baharini.

## Pamba Jiji yacheza mechi 9 bila ushindi

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha bao 1-0 kutoka kwa Tabora United ilichokipata kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, kimeifanya Pamba Jiji kuweka rekodi ya aina ya kucheza michezo tisa ya Ligi Kuu Tanzania Bara bila kupata ushindi.

Takwimu zinaonyesha haijawahi kutokea kwa misimu 10 ya Ligi Kuu Bara kwa timu kucheza idadi hiyo ya mechi bila kupata ushindi.

Hata hivyo, Kocha Mkuu, Fred Minziro, amewataka mashabiki wa timu hiyo kuwa wavumilivu kwa sababu ameanza kutengeneza kikosi chenye upinzani baada ya kubeba mikoba wa Mserbia Goran Copunovic.

"Nina siku chache tu tangu nitue hapa, tulivyocheza mechi iliyopita na leo (juzi), ni vitu viwili tofauti kabisa, leo (juzi), wachezaji walikuwa na nidhamu," alisema Minziro ambaye ameongoza timu hiyo kwa michezo miwili sasa.

Katika michezo tisa ambayo timu hiyo imecheza, imetoka sare mitano na kupoteza minne, ikiwa na pointi tano, ikikamata nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

## Polisi yaipunguza kasi Mtibwa Sugar

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi michezo minne mfululizo, Mtibwa Sugar ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi ya Championship iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi mkoani, Kilimanjaro juzi.

Wakati Polisi Tanzania ikishuka daraja msimu wa 2022/23, Mtibwa Sugar ilishuka msimu uliopita, hivyo mchezo wa juzi ulikuwa ni kama wa Ligi Kuu, ndani ya Championship.

Polisi Tanzania walianza kupata bao la kwanza lililofungwa na Farid Kupanda dakika ya 32, likiwa pia ni bao la kwanza ambalo Mtibwa Sugar wameruhusu katika nyavu zake.

Wageni walisawazisha dakika ya 38 kupitia kwa Raizin Hafidh, mchezaji bora wa Septemba wa Ligi ya Championship, lakini pia akiendelea kuongeza akaunti ya mabao baada ya kufikisha magoli matano na kuendelea kuwa kinara.

Pamoja na kupoteza mchezo huo, bado Mtibwa inaendelea kuongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 13, ikishinda minne na sare moja, huku Polisi Tanzania ikiwa nafasi ya 12 kwa michezo mitano ikiwa na pointi tano huku Stand United ikikwea hadi nafasi ya pili baada ya kuifunga Bigman FC bao 1-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Kambarage mkoani, Shinyanga.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**GYOKERES KUMRITHI HAALAND**

KLABU ya Manchester City inatazamia kumnunua mshambuliaji wa Sporting na Timu ya Taifa ya Sweden, Viktor Gyokeres, mwenye umri wa miaka 26, kama mbadala wa muda mrefu wa Erling Haaland. ***(Sky Sport Switzerland, via Mirror)***

**RAPHINHA ATAJWA UNITED**

KOCHA wa zamani wa Barcelona, Xavi anataka kumleta Old Trafford winga wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27 ikiwa atachukua nafasi ya Erik ten Hag kama Mkufunzi wa Manchester United. ***(Fichajes)***

**ANTONY KUREJEA AJAX**

WINGA wa Manchester United Mbrazil Antony mwenye umri wa miaka 27, anaweza kupewa fursa ya kuondoka Old Trafford na kurejea katika klabu yake ya zamani Ajax, lakini wababe hao wa Uholanzi wanasemekana hawajaridhishwa na mpango huo. ***(De Telegraaf)***

**ZYCH SASA KIMEELEWEKA**

KLABU ya Aston Villa iko tayari kumpa mlinda mlango wa Timu ya Taifa ya Poland, Oliwier Zych, 20, mkataba mpya huku Arsenal na Brighton wakiripotiwa kumtaka nyota huyo. ***(Football Insider)***

**ESQUIVEL ANUKIA BARCA**

BARCELONA wanamfuatilia mshambuliaji wa River Plate, ambaye ni raia wa Argentina, Felipe Esquivel, 16. ***(Sport)***

**MADRID KUMSAJILI TRENT**

REAL Madrid wanapanga kumpa beki wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Trent Alexander-Arnold, mwemye umri wa miaka 26 mkataba wa kati ya euro milioni 14 hadi 15. (Caught Offside)

**GUARDIOLA AMTAKA LUKEBA**

PEP Guardiola ameiomba Manchester City kumfuatilia beki wa RB Leipzig, Castello Lukeba, mwenye umri wa miaka 21, huku mkufunzi huyo wa Manchester City akitamani kumnunua Mfaransa huyo msimu ujao. ***(Fichajes)***

**BARCA, ARSENAL VITANI**

BARCELONA na Arsenal zinavutiwa sana na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia na Aston Villa, Jhon Duran, mwenye umri wa miaka 20, na Washikabunduki hao wanaweza kuwa katika nafasi nzuri zaidi kumsajili nyota huyo. ***(Fichajes)***


**CHUKWUEZE KUTUA EVERTON**

KLABU ya Everton inapanga kumsajili winga wa AC Milan kutoka Nigeria, Samuel Chukwueze, mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

**UNITED YAMFUATA DAVIES**

KLABU ya Manchester United inalenga kumshawishi beki wa pembeni wa Bayern Munich, Alphonso Davies, mwenye umri wa miaka 23. ***(Fichaje)***

## DONDO… SOKA
## MAGAZE… ULAYA




# BAO LA HAALAND SI LA KAWAIDA - GUARDIOLA

**MANCHESTER,** England

### Kocha huyo asema haelewi namna straika huyo alivyofunga...

PEP Guardiola amesema bao la Erling Haaland wakati Manchester City ikipata ushindi wa magoli 5-0 dhidi ya Sparta Prague "sio la kawaida kwa mwanadamu."

**Haaland alimalizia krosi ya Savinho katika kipindi cha pili kwa mpira wa kisigino.**

Raia huyo wa Norway alifunga tena kabla ya kubadilishwa na kufikisha mabao 44 katika mechi 42 za Ligi ya Mabingwa Ulaya na kujivuta hadi nafasi ya 16 kwenye orodha ya wafungaji wa muda wote.

"Sikujua jinsi alivyofunga," alisema Guardiola. "Kwa mwanadamu, ningesema hapana sio kawaida. Alifunga bao la ajabu.

"Anaweza kugusa mipira 15 au 20 lakini akapata nafasi saba au nane.

"Alifunga bao la ajabu, sawa na hili dhidi ya Borussia Dortmund miaka michache iliyopita. Sijui ni lipi gumu zaidi lakini nitasema yote mawili."

Mchezaji mwenzake wa Haaland wa City, Matheus Nunes, pia alishangaa.

"Ni bao la kushangaza. Nilikosa la kusema baada ya hapo," alisema Nunes akiimbia TNT Sports.

"Alipofunga bao kama hilo dhidi ya Dortmund nilikuwa nikitazama kwenye TV, kwa hiyo nimeoma moja kwa moja, ilikuwa ya kushangaza."

Kocha wa Sparta Prague, Lars Friis, pia alimwaga sifa kwa Haaland, ambaye tayari amefikisha mabao 13 kwa msimu huu.

"Unaweza kusema nini, labda ndiye mshambuliaji bora zaidi duniani," alisema Friis.

Ushindi wa City uliwapandisha hadi nafasi ya tatu kwenye jedwali la Ligi ya Mabingwa na kukaribia hatua ya mtoano kabla ya mechi dhidi ya Sporting CP na Feyenoord.

## HABARI MICHEZO




# RAPHINHA: TUMEWALIPIA KISASI MASHABIKI WETU

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Raphinha, amesema ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Bayern Munich katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ulikuwa ni "kuwalipia kisasi" mashabiki wa klabu hiyo kwa matokeo ya awali dhidi ya wababe hao wa Ujerumani.

Raphinha alifunga hat-trick katika mechi yake ya 100 akiwa na Barca huku klabu hiyo ya Katalunya ikimaliza msururu wa vipigo sita mfululizo dhidi ya Bayern Munich kwenye mashindano hayo.

Mbrazil huyo alikuwapo kwa mechi mbili tu kati ya hizo, na hakuwa amesaini Barca wakati walifungwa magoli 8-2 na Bayern Munich mechi iliyochezwa mwaka 2020, lakini alisema alizipitia zote kama shabiki.

"Ilikuwa kulipa kisasi," alisema Raphinha baada ya mchezo huo.

"Kwetu sisi ndani, wachezaji, hatuangalii yaliyopita. Tunaangazia mchezo unaofuata. Lakini niliteseka na michezo hiyo kama shabiki.

"Umekuwa usiku wa kustaajabisha na maalum, kufunga hat-trick katika mchezo wangu wa 100 kwa klabu. Nina furaha sana na jinsi tulivyocheza.

"Kama timu, tulicheza vizuri sana na hilo ndilo jambo muhimu zaidi kwangu. Kupata ushindi huo wa pili katika Ligi ya Mabingwa Ulaya ilikuwa muhimu."

Barca na Bayern walishuka dimbani kwenye Uwanja wa Olympic wakiwa na ushindi mmoja na kupoteza mmoja kutoka kwa mechi zao za ufunguzi katika Ligi ya Mabingwa msimu huu, na hivyo kulazimika kutopoteza pointi zaidi kutokana na kutokuwa na uhakika wa alama ngapi zitahitajika ili kusonga mbele.

Raphinha alifunga bao la kwanza dakika ya mwanzo, lakini Harry Kane, aliisawazishia Bayern kwa bao lake la 14 msimu huu katika mashindano yote.



# Slot aendeleza rekodi Liverpool

**LIVERPOOL,** England

KUANZA kwa msimu bila kuchoka kwa Liverpool chini ya kocha mpya, Arne Slot, kunaifanya timu hiyo kuvuka rekodi baada ya rekodi.

Liverpool walipata ushindi wa 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig juzi, moja ya klabu ambazo kocha wa zamani, Jurgen Klopp, ambaye hivi karibuni aliondoka kwa Wekundu hao baada ya karibu miaka tisa aliwahi kuziongoza.

Wachache walifikiri Slot angekuwa chini ya shinikizo huko Liverpool, lakini sasa Liverpool imeshinda mechi sita za ufunguzi za msimu mmoja za ugenini kwa mara ya kwanza katika historia ya miaka 132 ya klabu hiyo na Slot ndiye kocha wa kwanza kushinda mechi nyingi ambazo ni 11 kati ya 12 za kwanza akiwa katika mashindano yote.

Mholanzi huyo tayari ameiongoza Liverpool hadi kileleni mwa Ligi Kuu England akishinda mechi nane hadi sasa.

Ushindi wa tatu mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya umewaacha Liverpool kama moja ya timu mbili pekee pamoja na Aston Villa kuwa na pointi tisa hadi sasa.

"Makocha wengi wakubwa wamekuwa kwenye klabu hii," alisema Slot.

"Kwa hiyo ikiwa unaweza kufikia kitu ambacho hakijapatikana hapo awali, ni vigumu sana katika klabu kubwa kama hii.

"Rekodi ni nzuri, lakini kuna kitu kingine ambacho ni kizuri zaidi kuliko rekodi na sote tunajua ninachomaanisha ni ushindi."

# Barca kuivaa Atlético Miami

**MADRID,** Hispania

LALIGA inaendelea kufanya kazi katika kupanga mechi ya nyumbani ya Barcelona dhidi ya Atlético Madrid huko Miami nchini Marekani wikendi ya tatu ya Desemba, lakini mambo kadhaa bado yanahitaji kuwekwa ili mpango huo uendelee, vyanzo mbalimbali viliiambia ESPN.

Ligi ya Hispania imekuwa ikifanyia kazi kupeleka mchezo Marekani kwa miaka kadhaa, lakini hapo awali ilikabiliwa na upinzani kutoka Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF) na (FIFA).

Hata hivyo, vyanzo vinasema baadhi ya masuala hayo sasa yamewekwa sawa na kuna uwezekano wa kupeleka mchezo wa Barca dhidi ya Atlético kwenye Uwanja wa Hard Rock.

Relevent Sports Group, ambao wanafanya kazi katika mradi huo kwa ushirikiano na LaLiga, hawakutoa maoni yoyote juu ya maendeleo ya hivi sasa.

Chanzo kutoka FIFA kilikiri LaLiga na klabu zinafanyia kazi mpango huo lakini haikuweka wazi msimamo mpya.

Rais wa LaLiga, Javier Tebas, amesema mara kwa mara juu ya nia yake ya kucheza mchezo mmoja wa msimu nje ya nchi.

Barca na Atlético zote zimehusika katika mipango ya awali ya kupeleka mchezo Marekani.



HABARI MICHEZO

## Simba, Namungo

INATOKA UK. 24

ikawakosa nyota wake mbalimbali akiwamo beki wa kati, Abdulrazaq Hamza, Yusuph Kagoma na Charles Ahoua, ambao ni majeruhi.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazochezwa leo ni kati ya Singida Black Stars dhidi ya Fountain Gate huku KenGold wakiwafuata Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. Singida Black Stars yenye pointi 19 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga iliyofikisha pointi 18 wakati Simba iko katika nafasi ya tatu na pointi zake 16 kibindoni sawa na Fountain Gate.

Kagera Sugar yenye pointi tano sawa na Pamba Jiji FC na KenGold yenye pointi nne zinaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

## Gamondi aahidi ushindi Yanga kesho palepale

INATOKA UK. 24

mabingwa hilo liko wazi, wana kikosi imara, lakini na sisi tutafanya kila linazowezekana ili kupata ushindi, hivyo mchezo utakuwa mgumu kwa pande zote.

Nilipokuwa Ihefu nilikuwa naifunga Yanga, sidhani kama kuna mbinu mpya sana wanazo, kwa hiyo najua jinsi gani ya kudili nao, mbinu zilezile nilizokuwa natumia nilipokuwa Ihefu ndiyo nitazileta Coastal Union," Mwambusi alisema.

Wakati akiwa Mbeya City, aliifanya timu tishio kwa vigogo wa soka nchini, Simba, Yanga na Azam FC, na alipokuwa Ihefu, aliifanya kuwa timu pekee ambayo ilikuwa ikiisumbua Yanga.

Kuhusu kibarua chake katika timu hiyo, alisema alipokea kwa mikono miwili na kuahidi mazuri kwa sababu amepumzika muda mrefu na ameongeza mbinu mpya za kisasa za ufundishaji.

"Nimepokea kwa mikono miwili, walinitaka nikawaambia vitu ninavyohitaji wakanitekelezea. Ikumbukwe msimu wa 2022/2023 nilikuwa na kikosi cha Ihefu, nimepumzika msimu mmoja tu, nilipumzika huku nikijiimarisha kutafuta mbimu mpya," aliongeza kocha huyo.

Mwambusi anachukua nafasi ya David Ouma, ambaye aliondoshwa kwenye kikosi hicho kabla hata kuanza kwa msimu huu kutokana na timu hiyo kuondolewa mapema kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola ambayo kwa sasa ipo kundi moja na Simba katika mashindano hayo.

# MWAMBUSI AIMARISHA ULINZI COASTAL UNION, AITISHA YANGA



Na Shufaa Lyimo

KOCHA mpya wa Coastal Union, Juma Mwambusi, amesema ameanza na mazoezi maalumu ya kuisuka upya safu ya ulinzi ya timu hiyo ili isiruhusu mabao katika mechi dhidi ya Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwambusi alisema amewataka wachezaji wake waingie katika mechi hiyo kwa tahadhari kwa sababu wanakutana na timu ambayo haijapoteza mchezo hata mmoja.

"Nataka kujenga heshima kwa kuifunga Yanga katika mchezo wetu huo ambao ninaamini utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa, timu hizi zinapokutana mchezo hauwezi kuwa mwepesi, mchezo huwa na ushindani wakati wote," alisema Mwambusi.

Kocha huyo alisema pia amefuatilia michezo iliyopita ya timu yake na kuongeza hajaridhishwa na kasi iliyokuwa inaonyeshwa na safu ya ushambuliaji, hivyo kuifanyia marekebisho ili ipate nafasi ya kuifunga Yanga.

**Aliongeza malengo yake ni kupata pointi tatu katika mchezo wake huo wa kwanza akiwa ndani ya kikosi hicho.**

"Tunaendelea vizuri na mazoezi, ninashukuru mpaka sasa hakuna mchezaji yoyote ambaye ni majeruhi jambo ambalo linampa matumaini makubwa. Kila mchezaji yuko tayari kwa mchezo huo wa Jumamosi, wanafahamu hautakuwa mwepesi kwa kila upande kutokana na historia ya timu hizi," Mwambusi alisema.

Aidha Mwambusi amewaomba mashabiki wao kuendelea kujitokeza kuwashangilia kwa sababu hali hiyo inawaongezea hamasa ya kupambana kusaka matokeo mazuri.

"Tunaomba mashabiki waendelee kutupa ushirikiano, wajitokeze kwa wingi uwanjani ili tutimize mipango yetu, tumejipanga kuwapa furaha," Mwambusi alisema.



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa nyota wanaocheza ndani (CHAN), dhidi ya Sudan itakayochezwa Mauritani keshokutwa. **PICHA: TFF**

# *Che Malone: Tutalipa kisasi*




Na Faustine Feliciane

BEKI wa kati wa Simba, Che Malone Fondoh, amesema kupoteza mchezo dhidi ya Yanga kumewaumiza lakini wanaamini zamu yao ya kufurahi haipo mbali kwa sababu kikosi chao kinaendelea kuimarika.

Malone, aliliambia gazeti hili viwango vya wachezaji wa Simba vinazidi 'kupanda' na anaamini mechi ya marudiano dhidi ya Yanga watapata ushindi.

"Mchezo dhidi ya Yanga umepita, najua mashabiki wameumia kama ambavyo na sisi wachezaji tulivyoumia, lakini timu yetu inaimarika na tunapambana, hatupo mbali na mafanikio," alisema Fondoh.

Beki huyo alisema kwa sasa malengo yao ni kuhakikisha wanapata alama tatu katika kila mechi iliyoko mbele na hiyo inaendelea kupandisha viwango vyao.

"Hata ukiangalia mazingira ya goli tulilofungwa, ni bahati mbaya, lakini tumerejea mazoezini na kusahau yaliyopita na kupata ushindi mchezo wetu uliofuata dhidi ya Prisons...kwa sasa akili zetu tumeelekeza kuikabili Namungo," alisema Malone.

Nyota huyo ndiye alifunga bao pekee katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine na Malone alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo.

Simba leo itakuwa mwenyeji wa Namungo FC kwenye Uwanja wa KMC, Complex Dar es Salaam.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 25, 2024

Nipashe





Bao la Haaland si la kawaida UKURASA 21

# Simba SC, Namungo kazini Bara

## ●●● Kocha Fadlu atamba ushindi upo, lakini awataka mashabiki...

**Na Faustine Feliciane**

KIKOSI kinazidi kuimarika, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Wekundu wa Mismbazi, Fadlu Davids, ambao wanatarajia kuwakaribisha Namungo FC kutoka mkoani Lindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Fadlu, alisema wachezaji wake wako tayari kuwakabili wapinzani wao na anafurahishwa na viwango vya nyota wake kuelekea mchezo huo.**

Fadlu alisema kikosi chake kinaendelea kuimarika kutoka mchezo mmoja hadi mwingine na amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuwa wavumilivu kwa sababu muda si mrefu wataiona timu wanayoitaka.

Kocha huyo alisema tangu ameanza kuifundisha timu hiyo anaona mabadiliko makubwa akilinganisha na wakati anaipokea.

Aliongeza kuelekea mchezo wa leo, hatarajii kuona mechi rahisi lakini ushindi walioupata dhidi ya Prisons umeongeza hali ya kujiamini na hamasa ya kuwavaa Namungo.

"Lengo letu la kwanza ni ushindi, nafahamu Namungo ni timu nzuri, lakini tunahitaji pointi tatu, nadhani kikosi changu kitakuwa na mabadiliko kidogo kutokana na baadhi ya wachezaji wengine kuwa majeruhi.

Tuna timu nzuri, wachezaji wanaendelea kuonyesha uwezo mkubwa kiuchezaji, tumetoka kucheza mchezo mgumu ugenini dhidi ya Prisons, tumepata ushindi na tumecheza vizuri, muda mchache ujao timu itakuwa kwenye kiwango cha juu sana," alisema Fadlu.

Kocha huyo raia wa Afrika Kusini alisema muhimu kwake kwa sasa ni kuendelea kujenga kikosi imara ambacho kitaonyesha kiwango cha juu zaidi katika kila mechi watakayocheza.

"Ninaiona Simba ya tofauti sana siku chache zijazo, napenda namna wachezaji wangu wanavyopambana na wanavyoonyesha wana uchu na kiu ya mafanikio, hili ni jambo zuri sana, kama mwalimu ninaridhishwa na kile ninachokishuhudia kutoka kwa kila mchezaji," Fadlu aliongeza.

Naye Kocha Msaidizi Namungo, Ngawina, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vizuri kukabiliana na wapinzani wao.

Ngawina alisema wanaifahamu vyema Simba na wamejipanga kuwadhibiti lakini pia wakicheza kwa tahadhari.

"Tunaiheshimu Simba, ni timu kubwa na inawachezaji wazuri, lakini tumekuja kujaribu kuondoka na pointi zote tatu, tutacheza kwa nidhamu kuhakikisha haturuhusu kufungwa na sisi tupate ushindi," alisema Ngawina.

Hata hivyo Ngawina leo atakuwa chini ya kocha mpya, Juma Mgunda, ambaye ametangazwa rasmi kuchukua mikoba ya Mwinyi Zahera, aliyepangiwa majukumu mengine.

Mgunda leo ataanza kuiongoza kwa mara ya kwanza dhidi ya waajiri wake wa zamani, baada ya kusaini mkataba wa kuitumikia timu hiyo.

Hata hivyo Mnyama huenda leo

INAENDELEA UKURASA 23




Kibu Denis

# Gamondi aahidi ushindi Yanga kesho palepale

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anataka kuona wanaendelea kasi ya ushindi watakapoivaa Coastal Union 'Wagosi wa Kaya' katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Hata hivyo amesema atatambulisha mfumo tofauti kwa sababu ya aina ya uwanja watakaocheza katika mechi hiyo ya kesho.

Gamondi, raia wa Argentina, amesema kikosi chake kwa sasa kimeanza kurejea katika kiwango ambacho anahitaji ingawa si kwa asilimia zote, huku baadhi ya wachezaji wake waliokuwa kwenye vikosi vya timu za taifa wakipata muda wa kupumzika.

"Nadhani sasa wachezaji wangu wamepata mapumziko kidogo, tunakwenda kucheza mchezo mwingine wa Ligi Kuu, tunatarajia kupata ushindi, ingawa si mwepesi, Coastal Union ni timu ambayo huwa inatupa tabu kidogo, nakumbuka msimu uliopita, tuliwafunga bao 1-0 katika kila mzunguko, kwa maana hiyo hautakuwa mchezo mwepesi," alisema Gamondi.

Yanga inakwenda kucheza mchezo huo ikiwa ndiyo timu pekee iliyoshinda kwa asilimia 100, ikicheza michezo sita na kushinda yote, lakini pia ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutikiswa msimu huu.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mwambusi, ameliambia gazeti hili ataingia uwanjani na staili ambayo alikuwa akiitumia alipokuwa akiifundisha Ihefu FC dhidi ya Wanajwangani hao.

Mwambusi alisema anafahamu Yanga ni timu bora kwa sasa nchini, lakini isitarajie kupata ushindi kirahisi kwa sababu yeye ndio kiboko yao.

"Kwa sasa ni muda mfupi tu kueleza lolote, tunajua Yanga ni timu nzuri kwa sababu ni

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >